

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TANO**

**Kikao cha Sita – Tarehe 7 Novemba, 2016**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**TANZIA**

Waheshimiwa Wabunge, nachukua fursa hii kwa masikitiko makubwa kuwajulisha rasmi kwamba Mzee Samuel John Sitta, Spika Mstaafu wa Bunge la Tisa, amefariki dunia usiku wa kuamkia leo, tarehe 7 Novemba, 2016 mnamo saa 7.50 time za Ujerumani, katika Hospitali ya *Clinic of Nuclear Medicine Technical University of Unique* iliyopo nchini Ujerumani ambapo alikuwa anapata matibabu.

Mheshimiwa Sitta aliondoka nchini tarehe 3 Novemba, 2016 na alikuwa nchini Ujerumani kwa ajili ya matibabu zaidi ambayo Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania ilikuwa inayagharamia.

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu natoa pole nyingi kwa familia hususan Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta wa Jimbo la Urambo ambaye ameondokewa na mumewe. Ofisi itaendelea kuwajulisha taarifa zaidi kuhusu msiba huu.

Waheshimiwa Wabunge naomba tusimame kwa dakika moja ili kutoa heshima ya Mzee Samuel Sitta,

Mwenyezi Mungu ailaze Roho yake Marehemu.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walisimama kwa dakika moja kuomboleza kifo cha Spika Mstaafu Marehemu Samuel John Sitta)*

**MWENYEKITI:** Ahsanteni, tukae. Katibu!

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MWEZANI:**

### **MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaanza maswali Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Mheshimiwa Deogratius Ngalawa.

Na. 54

### **Tatizo Kubwa la Maji - Ludewa**

**MHE. DEOGRATIUS F. NGALAWA** aliuliza:-

Pamoja na kwamba Jimbo la Ludewa lina vyanzo vingi vya maji, lakini kuna matatizo makubwa sana ya maji na wadau mbalimbali wamekuwa wakijitokeza kusaidia tatizo hili lakini Serikali na Halmashauri zimekuwa hazitoi ushirikiano kwa kurudi nyuma katika kuchangia sehemu yao kwa kigezo cha kutokuwa na fedha. Mfano vijiji vya Maholongwa, Mlangali, Mavanga, Manda, Nkomang'ombe na Lwela.

(a) Je, Serikali iko tayari kuweka kipaumbele katika kusaidia pale inapohitajika kuchangia?

(b) Je, nini kauli ya Serikali katika kushughulikia tatizo la maji Jimboni Ludewa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deogratius Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo unafanyika kwa njia shirikishi yaani Serikali, wadau wa maendeleo na wananchi kupitia mpango wa fursa na vikwazo kwa maendeleo. Kwa utaratibu huo mafanikio makubwa yamepatikana katika kuboresha huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2016/2017, Serikali imeweka kipaumbele na kutenga shilingi milioni 861 kwa ajili ya kukamilisha mradi wa maji katika Kijiji cha Lugarawa, ukarabati wa miradi ya maji Lifua/Manda na Kijiji cha Ludewa K. Vilevile Serikali inashirikiana na taasisi isiyo ya Kiserikali ya *Lusala Development Association* kwa ajili ya kukamilisha mradi wa maji katika vijiji vya Mlangali, Mavanga na Nkomang'ombe utakaogharimu shilingi milioni 250 ambapo mchango wa Serikali ni shilingi milioni 50.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapongeza mchango mkubwa wa wadau mbalimbali kushirikiana na wadau wa maendeleo katika sekta za maji zikiwemo taasisi za dini. Serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo na kuhakikisha bajeti inatengwa kila mwaka kwa ajili ya kutatua tatizo la maji kwa wananchi wa Ludewa na maeneo mengine hapa nchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngalawa.

**MHE. DEOGRATIUS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini bado tunauliza. Wadau mbalimbali wamekuwa wakichangia michango hii ya maji kwa karibu sana lakini Serikali imekuwa ikusuasua kupeleka hizi hela.

Je, Mheshimiwa Waziri ananithibitishiaje kwamba tutazipata fedha hizi kwa haraka?

Pili, kwa sababu wadau wa maendeleo wamekuwa wakileta ile michango na kazi inakuwa imeshafanyika, kutokana na Serikali kuchelewesha michango yao inakuta kwamba baadhi ya miundombinu inakuwa tayari imeshabomoka.

Je, Serikali inaweza ikagharamia ile miundombinu iliyobomoka kwa sababu ya kuchelewesha kwa fedha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS-TAMISEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze wazi kwa sababu Serikali kuna *commitment* ya shilingi milioni 50, na kwa sababu jukumu letu kubwa ni kuhakikisha miradi ya maji iliyotengwa katika kipindi hichi inaweza ikapata msaada wa haraka. Naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Deogratius, ofisi yetu itafanya kila liwezekanalo kuhakikisha tunasukuma pesa hii milioni 50, kama ni *matching grants* ya kuhakikisha mradi huo unatekelezeka, tutaweza kulifanya hili wala usihofu, mimi mwenyewe naomba nitoe *commitment* hiyo kama Serikali kuhakikisha jambo hili linakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima kwamba miradi mingine imetekelezwa lakini mpaka imechakaa. Je, ni nini kauli ya Serikali kuhakikisha miradi ile sasa inarekebishwa kuweza kufanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Deo kuwa tutakachokifanya kwanza ofisi yetu itawasiliana na Ofisi wa RAS Mkoa wa Njombe, kuangalia ni jinsi gani kama kuna miradi ambayo ina changamoto kubwa na kubainisha ni kitu gani kinatakiwa kifanyike. Kwa sababu mwisho wa siku, mradi kama umetekelezwa lakini mradi saa nyingine umeharibika kabla ya kuwapatia wananchi fursa hiyo ya maji ina maana tutakuwa hatujafikia malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Ofisi ya RAS Mkoa wa Njombe naomba niagize kupitia mkutano huu, kwamba wahakikishe wanafanya *follow up* katika Jimbo hili la Ludewa kuangalia changamoto iliyokuwepo halafu tuangalie mkakati sasa, tutafanyaje ili mradi miradi hiyo iweze kufanya kazi. Lengo kubwa wananchi wako Mheshimiwa Deo waweze kupata fursa ya maji, na hiyo ndio azma ya Serikali kwamba kuhakikisha inawahudumia wananchi wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi ili kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida ya maji katika Jimbo la Ludewa inafanana sana na shida ya maji katika Jimbo la Ukonga. Ukitembelea kata za Kivule, Msongola, Chanika, Buyuni, Zingiziwa, Pugu, *Pugu Station*, Ukonga, Gongo la Mboto na Kipunguni. Kata hizi zote hazina maji kabisa na hasa maji ambayo yanasimamiwa na Serikali ambayo ni maji safi na salama.

Sasa nilikuwa naomba kuuliza, kwa sababu nimezungumza mara nyingi Bungeni hapa kuuliza shida ya maji Dar es Salaam na hasa Jimbo la Ukonga ni nini kauli ya Serikali na hasa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana kwamba baada ya Bunge hili tuongozane kwenda Ukonga akashuhudie watu wa Ukonga wanavyokunywa maji machafu na hasa kwenye shule, zahanati na vituo vya afya? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu. Mheshimiwa Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Jimbo la Ukonga lina changamoto ya upatikanaji wa maji. Lakini tunayo mipango ambayo inayoendelea katika Mpango wa Utekelezaji wa Programu *Phase II* ipo miradi ambayo Jimbo la Ukonga wametengewa fedha. Lakini katika mpango

wa muda mrefu, maeneo ya Ukonga, Mkaranga na maeneo ya Kigamboni, maji yatapatikana kutoka chanzo cha Mpera na Kimbiji. Ambapo sasa utekelezaji wake tumeanza kuchimba visima karibu visima 20 vinakamilika. Baada ya hapo tunajenga miundombinu ambayo tutapeleka maeneo hayo ya Ukonga na kutakuwa hakuna tatizo kubwa na nikuahidi kwamba katika kipindi cha miaka hii minne ambayo imebakia katika Seriali ya Awamu ya Tano, tutahakikisha kwamba Ukonga inakuwa na maji ya kutosha.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Ishengoma!

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mradi wa maji ni tatizo kweli, katika Wilaya ya Morogoro Vijijini, katika vijiji vya Furwe, Mikese, Gwata walihidiwa mradi wa maji kwa muda wa miaka mingi, na wananchi wanateseka kwa maji kwa muda mrefu. Je, naomba kuuliza wananchi hawa ambao wameteseka kwa muda na wamehidiwa mradi wa maji watapata lini maji na mradi huu utatekelezwa lini?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshatoa maelekezo katika kila Halmashauri namna ya kupanga vipaumbele katika vijiji ambavyo havina maji; sasa awamu hii ya kwanza siwezi kusema ni vijiji vipi vimepangwa, lakini Halmashauri yake inafahamu na wameleta vipaumbele na tumeweka kwenye bajeti na fedha zimetengwa. Kwa hiyo, sasa hivi ni ufuatilia tu utekelezaji, naomba nimuahidi Mheshimiwa Mbunge nitakaa naye ili kusudi niweze kuona hivyo vijiji anavyovisema vipo kwenye mpango wa mwaka huu au vipi, ili tuweze kuona namna ya kufanya.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Fedha na Mipango, swali la Mheshimiwa Hassan Selemani Kaunje.

Na. 55

### **Kuangalia Upya Takwimu za Watu Jimbo la Lindi**

**MHE. HASSAN S. KAUNJE** aliuliza:-

Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 inasema kuwa idadi ya watu katika Jimbo la Lindi Mjini ni takribani 78,000, lakini takwimu za watu waliojiandikisha NIDA inafika 100,000 na sensa iliyofanywa kupitia Serikali za Mitaa inaonyesha kuwa wakazi wa Lindi Mjini ni zaidi ya 200,000 na Serikali inaendelea kupanga mipango yake ya maendeleo kwa kutumia takwimu za watu 78,000 hivyo kuathiri huduma stahiki za maendeleo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuangalia upya takwimu hizo ili wananchi wa Lindi Mjini wapelekewe huduma za maendeleo stahiki?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Kaunje, Mbunge wa Lindi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, idadi ya watu kwa Manispaa ya Lindi (Jimbo la Lindi Mjini) ilikuwa ni watu wapatao 78,841. Kwa madhumuni ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, eneo la Manispaa ya Lindi ni lile linalojumuisha kata 18 za Ndoro, Makonde, Mikumbi, Mitandi, Rahaleo, Mwenge, Matopeni, Wailes, Nachingwea, Rasbura, Matanda, Jamhuri, Msinjahili, Mingoyo, Ng'apa, Tandangongoro, Chikonji na Mbanja. Hivyo basi, tunapozungumzia idadi ya watu 78,841 tuna maana ya idadi ya watu katika kata nilizoitaja hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uboreshaji wa daftari la wapiga kura, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilitoa makadirio ya idadi ya wapiga kura kwa kila jimbo hapa nchini. Katika makadirio hayo, Jimbo la Lindi Mjini linakadiriwa kuwa na wapiga kura 47,356. Katika zoezi hilo hilo la uboreshaji wa daftari la wapiga kura, Tume ya Taifa ya Uchaguzi nayo ilikadiriwa kuwa Jimbo la Lindi Mjini lina wapiga kura wapatao 42,620. Makadirio haya yalizingatia idadi ya watu kwa Lindi Mjini kama ilivyotolewa na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012.

Baada ya kukamilika kwa zoezi la uandikishaji wapiga kura, Jimbo la Lindi lilionyesha kuwa na wapiga kura 48,850 idadi ambayo ni karibu sawa na ile iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Matokeo haya yanadhihirisha usahihi wa takwimu za sense zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya watu wapatao 100,000 waliojiandikisha NIDA ni kwa Wilaya nzima ya Lindi, ambayo inajumuisha Manispaa ya Lindi na Halmashauri ya Wilaya ya Lindi na sio Manispaa ya Lindi au Jimbo la Lindi Mjini pekee kama ilivyohojiwa katika swali la msingi la Mheshimiwa Hassan Kaunje.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaunje.

**MHE. HASSAN S. KAUNJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nisikitike tu kwamba jibu lake haliendani na uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhalisia uliokuwapo Lindi ni kwamba takwimu za watu wanaokadiriwa 100,000 ni wa Jimbo la Lindi Mjini. Vilevile nimkumbushe Naibu Waziri katika mchakato wa bajeti iliyopita ya mwaka jana kwamba maafisa wa Halmashauri walishakaa vikao tofauti na maafisa wa Wizara yake katika kuangalia uwezekano wa kubadili bajeti kutokana na idadi ya watu. Sasa anaposema kwamba idadi ya wakazi wa Lindi na akitumia takwimu za wapiga kura ni sahihi nakataa kukubali jibu lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize maswali ya nyongeza kama tu Mheshimiwa Naibu Waziri na Wizara yake walikubali kwamba idadi ya watu wa Lindi ni kidogo na hivyo watafanyia kazi mchakato wa kuongeza bajeti katika bajeti inayokuja, je, yuko tayari kuthibitisha hilo au kulifanyia kazi hilo kwa bajeti inayokuja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kutokana na idadi ya watu kutotumika idadi stahiki katika Jimbo la Lindi imepelekea huduma za afya kupeleka katika kituo kimoja tu cha afya katika Lindi Mjini na hivyo kupeleka shida kubwa kwa watu wa Lindi.

Je, Mheshimiwa Waziri anayehusika yuko tayari kuiboresha hospitali inayotoa huduma ambayo inaendeshwa na Jeshi la Polisi Lindi ili kuweza ku-*accommodate* matatizo ya afya ya wananchi wa Jimbo la Lindi? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu wa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali la kwanza ambalo anasema kwa bajeti inayokuja, naomba nilikumbushe Bunge lako tukufu kwamba Bunge hili lilipitisha sheria ya takwimu Machi, 2015 ambayo inatoa mamlaka kwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu kuratibu takwimu zote rasmi. Na kwa Serikali tunachofahamu ni kwamba idadi ya watu wa Lindi Mjini ni ambao wametajwa na kwa makadirio ya mwaka 2016, idadi ya watu Lindi Mjini ni 85,871 hiyo ndio takwimu rasmi inayotambulika na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuhusu swali la pili, naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge swali hili tutakaa pamoja na Waziri wa Afya na Waziri wa TAMISEMI tutalifanyia kazi kuona hospitali hii inaboreshwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Nishati na Madini. Mheshimiwa Rhoda Kunchela kwa niaba Mheshimiwa Devotha Minja.

Na. 56

### **Ukosefu wa Umeme Wilaya ya Mpanda Mjini**

**MHE. DEVOTHA M. MINJA (K.n.y MHE. RHODA E. KUNCHELA)** aliuliza:-

Tatizo la umeme katika Mkoa wa Katavi hususan Wilaya ya Mpanda Mjini limekuwa kero kwa wananchi; tatizo hili linafanya maendeleo kuwa duni katika Manispaa ya Mpanda:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuachana na matumizi ya jenereta ambalo ni bovu linalosababisha ukosefu wa umeme kila mara?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua kero hii ya umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Gridi ya Taifa inayounganisha Mikoa ya Rukwa, Katavi pamoja na Kigoma. Ujenzi wa mradi huo utasaidia mikoa hiyo kuondokana na matumizi ya mitambo ya mafuta pia na gharama kubwa. Kwa maana hiyo ujenzi huo unahusisha njia ya umeme msongo wa kilovolti 400; ambao pia ambao pia wameanza kuunganisha katika mikoa Mbeya - Sumbawanga - Mpanda - Kigoma hadi Nyakanzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kuhuisha upembuzi yakinifu wa mradi kutoka kilovoti 220 za awali na kuwa kilovolti 400 zinazoendelea hivi sasa inaendelea. Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi (Mbeya - Sumbawanga) itakamilika mwaka, 2018 na awamu zote tatu za mradi zinatarajiwa kukamilika mwaka 2022; gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa dola za Marekani milioni 664.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu utakapokamilika utaupatia umeme wa uhakika Mji wa Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ujenzi wa umeme wa Gridi ya Taifa unaendelea, Serikali kupitia TANESCO imeanza ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia jenereta mbili zenye uwezo wa kuzalisha umeme wa megawati 1.25; kila moja katika Mji wa Mpanda kupitia mradi wa ORIO. Mradi huu unafadhiliwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Uholanzi kwa



gharama ya shilingi bilioni 12.21. Kazi za ujenzi wa kituo hicho zimeanza mwezi Oktoba, 2016 na zitakamilika mwezi Julai, 2017.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza Waziri kwa majibu yake, amesema mwaka 2018 ndio mradi huo utakamilika, ni nini *commitment* ya Serikali kwa kuwa hadi kufikia mwaka 2018 na wananchi wanaihitaji nishati hii muhimu kwa ajili ya maendeleo. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuangalia njia mbadala kuweza kusaidia wananchi hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa tatizo la nishati ya umeme katika Mkoa wa Katavi linafanana kabisa na matatizo ya umeme katika Mkoa wa Morogoro hasa katika Manispaa ya Morogoro katika Kata za Mindu, Kihonda na Mkundi ambapo wananchi hawa kwa muda mrefu hawana nishati ya umeme ingawa wanapitiwa na Gridi ya Taifa. Je, Serikali haioni kama kuna haja ya kuhakikisha wananchi hawa wanapata umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *commitment* ya Serikali kwa Mkoa wa Katavi pamoja na Sumbawanga kwa kweli ni kubwa sana. Hadi sasa mbali na mradi huu wa kupeleka umeme wa kilovolti 400 hivi sasa Serikali imeanza kukarabati majenereta mawili yaliyokuwa na matatizo pale Mpanda. Yale majenereta yalikuwa na uwezo wa megawati 2.6 lakini yalikuwa yanatoa umeme wa megawati 2.3, ukarabati wa majenereta hayo umekamilika tarehe 5 mwezi huu kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa Mpanda pamoja na maeneo ya jirani umeme utapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatua ya pili sasa hivi ujenzi umeanza kufunga jenereta mbili mpya ambazo pia zinatengenezwa, kama nilivyosema kwenye swali la msingi, kupitia mradi wa *ORIO*. Jenereta hizi zina uwezo wa kufua megawati 2.5 kwa ujumla wake kwa hiyo, Mji wa Mpanda pamoja na Sumbawanga sasa watakuwa na jumla ya megawati 5.1 ambapo matumizi yao kwa sasa hivi ni megawati 2.6. Kwa hiyo, vijiji vyote sasa vya Mchangani, Dilifu, Longililo, Mpakani, Gereza la Kakalankurukuru, pamoja na Kalamsenga vyote vitapata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na vijiji vya Morogoro vikiwemo Mindu pamoja na Kihonda, vijiji hivi vinapelekewa umeme kupitia mradi kabambe wa *REA* Awamu ya Tatu unaoanza tarehe 15 Disemba, 2016. Na vijiji vyote vya Kihonda na maeneo ya jirani ikiwemo pamoja na Mindu vitapelekewa umeme wa uhakika mwaka huu.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa REA inafanya kazi nzuri sana na imesambaza umeme karibu nchi nzima na Mpwapwa kuna vijiji ambavyo havijapata umeme, kijiji cha Kibojani, Mgoma, Mzogole, Viberewele, Sazima, Mkanana, Igoji Kaskazini na Igoji Kusini pamoja na Iwondo.

Je, Mheshimiwa Waziri, utakuwa tayari kupeleka umeme katika vijiji hivi kwa sababu umeme ndio uchumi wetu na ndio maendeleo yetu katika nchi yetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana kuna wengi wanataka kuuliza maswali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa tuko tayari kupeleka umeme kwenye vijiji vyote vya Mheshimiwa Lubeleje. Mheshimiwa Lubeleje ni Mbunge mkongwe, nadhani kati ya Wabunge wote ambao tuko hapa Mheshimiwa Lubeleje ni wa zamani sana kwa hiyo, hatuwezi kumuangusha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Lubeleje nikuhakikishie vijiji vyako vyote vya Lugoma na Kiwelewele vitapelekwa umeme kupitia REA Awamu ya Tatu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mlata, Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nilikuwa naomba kumuuliza Naibu Waziri kwa kuwa REA wamejitahidi sana kusambaza umeme vijijini, lakini TANESCO hawaingilii kwenda kuanza kusambaza umeme kwenye maeneo mengine ambayo yameanzishwa hasa ya uzalishaji, mfano Kata ya Gumanga kuna kiwanda cha kusindika nyanya, umeme haujapelekwa Mkalama. Nilikuwa naomba kuuliza ni kwa nini TANESCO sasa wasiende kuanza kusambaza umeme? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji alivyotaja Mheshimiwa Mlata kwanza kabisa viko kwenye Mpango wa REA, lakini sambamba na Mpango wa REA bado TANESCO wanapeleka nguzo. Nimhakikishie tarehe 15 mwezi uliopita Mheshimiwa Mlata tulimpelekea nguzo 20 za umeme ambazo zitafungwa kuanzia tarehe 20 mwezi unaokuja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mlata vijiji vyako vyote vya Manga pamoja na ulivyotaja Mkarama vitafungiwa umeme kupitia REA pamoja na TANESCO.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kunipa nafasi hii. Namuuliza swali Naibu Waziri, alipokuja Mpanda alituhakikishia wananchi wanaoishi vijiji vya Kabungu, Mchakamchaka, Ifukutwa na Majalila ambako ni Makao Makuu ya Wilaya kwamba ataleta umeme ifikapo mwezi wa tisa. Je, ni lini Serikali itathibitisha kauli yake ambayo aliitoa yeye mwenyewe alipofika huko?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa nilitembelea maeneo mengi sana katika Jimbo la Mheshimiwa Kakoso na hasa kabla ya kutaja maeneo ya Majalila, Mheshimiwa Kakoso kwanza nikuhakikishie Gereza lako la Kakalankurukuru ambalo lina miaka 37 halina umeme litapatiwa umeme mwezi ujao kupitia Mradi wa REA unaoanza mwezi ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitembelea pia Kata ya Majalila ambako kuna mitambo na miradi ya maji. Nikuhakikishie Mheshimiwa Kakoso, mradi wa REA utakapoanza kufikia mwezi Januari hadi Februari mwaka unaokuja mradi wako wa Majalila utafungiwa jenereta za umeme, lakini pia jenereta ya umeme itaunganishwa na umeme ambao sasa unapitia mradi wa REA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijiji cha Kabungu nilikitembelea pamoja na Mpanda Mji Mpya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kakoso nikuhakikishie, vijiji vyako vyote 32 vilivyobaki vitapatiwa umeme kupitia mradi wa REA kuanzia Disemba na Januari mwaka unaokuja.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuuliza swali Namba 57 naomba kufanya sahihisho dogo tu pale la kimaandishi, Kata za Lengatei, Kijungu na Maungu, siyo neno Maungu naomba ibadilishwe iwe Kata ya Magungu. Baada ya sahihisho hilo dogo naomba swali namba 57 lipate majibu ya Serikali.

Na. 57

### **Kupeleka Umeme wa REA Wilaya ya Kiteto**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA** aliuliza:-

Pamoja na juhudi za Serikali kupeleka huduma za umeme vijijiji vya Wilaya ya Kiteto hasa Kata za Lengatei, Kijungu, Magungu, Songambebe, Ndedo na Makame, hawajafikiwa kabisa na utaratibu huu wa REA.

Je, Serikali itapeleka lini umeme katika vijiji vilivyotajwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vya kata za Lengetai, Kijungu pamoja na Magungu, kama ambavyo amerekebisha Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Songambele, Ndedo na Makame vitapatiwa umeme kupitia mradi kabambe wa REA Awamu ya Tatu unaoanza kutekelezwa mwezi Disemba, mwaka huu. Ujenzi wa mradi huu utanza Disemba kama nilivyosema mwaka huu na utakamilika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, vijiji vya kata za Lengatei vikiwemo Ilala, Kijungu, Lesoit pamoja na kijiji cha Magomeni pia vitapatiwa umeme kupitia mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kupeleka umeme kwenye Wilaya ya Kiteto itahusisha ujenzi wa njia ya msongo wa kilovolti 33 yenye urefu wa kilometa 810. Ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovolti 0.4 yenye urefu wa kilometa 1,725 ufungaji wa transfoma 343 za ukubwa mbalimbali, lakini pia kuwaunganishia wateja wa awali umeme 10,800. Kazi hizi zitaanza mwezi Disemba mwaka huu na kukamilika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020. Gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni 51.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya kutia matumaini, naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kiteto kwa sehemu kubwa inakaliwa na jamii ya wafugaji ambao shule haijawa kipaumbele sana, hasa kwa watoto wa kike. Kwa sehemu kubwa ukombozi mkubwa ni kuwa na shule za bweni ambako wasichana wanaweza wakabaki shuleni badala ya kurudi nyumbani kukwepa kuolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosikitisha ni kwamba kuna baadhi ya sekondari za kata tena za muda mrefu zenye mabweni, kama sekondari ya Ndedo na Lesoit ambazo ni za bweni na zina wasichana wengi wa Kimasai, lakini inasikitisha kwamba hizo shule za kata hadi leo hazina umeme. Na sio hizo shule tu hata Kituo cha Afya cha Osteti ambacho kinasaidia sana huduma za afya kwa akina mama hakuna umeme.

Je, ni lini Naibu Waziri sasa atachukua jukumu la makusudi kutembelea Wilaya ya Kiteto, hasa maeneo haya niliyoyataja, ili kujionea mwenyewe jinsi ambavyo sekondari hizo hazina walimu na hata maabara tulizojenga hazitumiki kwa ajili ya kukosa umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, naomba ku-*declare interest* kwamba nimetoa mikopo kwa takribani miaka 20 sasa katika Mkoa wangu wa Manyara. Uzoefu unaonyesha kwamba ufanisi mkubwa kwa kurejesha mikopo kwa wanawake na vijana ni katika vijiji vile vyenye umeme wa uhakika. Je, nini kauli ya Serikali kabla ya kutoa hizo shilingi milioni 50 katika maeneo haya ya wafugaji na mikoa ya pembezoni kuhakikisha kwamba vijiji hivyo vitakuwa na umeme kabla ya kusambaza hizo fedha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi. Jiandae Mheshimiwa Shekilindi, Mheshimiwa Silinde.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Mradi wa REA Awamu ya Pili ulipokamilika maeneo mengi sana ya taasisi hayakupatiwa umeme. Nitoe rai tu kwamba, REA Awamu ya Tatu inayoanza sasa itaweka kipaumbele sana kupeleka umeme kwenye taasisi za umma ikiwemo shule, sekondari, pamoja na taasisi nyingine. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Umbulla kwamba, shule ya sekondari ambayo ameitaja Lesoit pamoja na shule ya Ndedo pamoja na Kituo cha Afya cha Osteti vitaanza kabisa kupelekwa umeme kwenye mradi wa REA Awamu ya Tatu unaoanza hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nimpongeze tu Mheshimiwa Mbunge, amekuwa akifuatilia sana masuala haya, lakini nimhakikishie mbali na vituo vya afya kwa sababu viko vingi. Viko vituo vya afya katika eneo lake la Njiapanda ambako pia kuna kituo cha afya kitawekwa umeme, lakini kuna eneo la Songambeke halijawekwa umeme pamoja na vituo vingi sana ikiwemo na vijiji vya katikati na vyenyewe vitapatiwa umeme katika REA Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda kutembelea, kwa ridhaa yako, mara baada ya Bunge tufuatane na Mheshimiwa Mbunge moja kwa moja ikwezekana tuanze kukaa hata kabla ya kuanza kutembelea maeneo yake.

Kuhusiana na vijiji ambavyo vitapewa mikopo au ruzuku ya shilingi milioni 50 kupata umeme. Tutaanza kuvipatia umeme, tutakaa na wenzetu wa TAMISEMI ili kusudi shilingi milioni 50 zisiende bure, ili waanze kutumia umeme mara watakapoanza kupata pesa hizo.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi, ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mradi wa REA Awamu ya Pili umeshapita baadhi ya maeneo tena ya barabarani katika Jimbo la Lushoto. Je, Serikali inaniahidi lini itapeleka

umeme wa REA Awamu ya Tatu hasa katika Kata za Kilole, Kwekanga, Makanya, Ngwelo pamoja na maeneo mengine yaliyobaki?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kusema tu Mradi wa REA Awamu ya Tatu unapeleka umeme katika vijiji vyote, katika vitongoji vyote na katika taasisi zote za umma, lakini hata miji ambayo pia, iko *isolated*. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kijiji chake cha Kilole kitapelekewa umeme hata kijiji cha Makanya kitapelekewa umeme kwa sababu, ni mpango wa Serikali kupeleka umeme katika vijiji vyote kupitia REA Awamu ya Tatu.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kabla ya kuanza kwa Mradi wa REA III, kuna baadhi ya maeneo Miradi ya REA I na REA II bado haijakamilika ikiwemo katika baadhi ya maeneo ya Jimbo la Momba. Sasa tunataka *assurance* ya kukamilisha miradi kwanza ya REA I na REA II kabla ya hiyo REA III, lini itakamilika miradi hii, REA I na REA II? Ahsante Sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Silinde kwanza nakupongeza, Miradi ya Awamu ya Pili ya REA imeshakamilika na mahali ambapo Mradi wa REA ikitokea kwamba haukukamilika ni vijiji ambavyo sasa vitaanza kutekelezwa katika Miradi ya REA Awamu ya Tatu.

Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Silinde kama kuna kijiji *specific* ambacho hakijakamilika kupitia mradi wa pili, naomba tukae na tuanze kutekeleza hata kabla ya kuingia Mradi wa REA Awamu ya Tatu. Na vijiji vyote ambavyo havikukamilika kupitia miradi ya REA Awamu ya Pili, ambavyo havijakamilika, vitaanza kukamilika kwanza ndio tunaingia kwenye REA Awamu ya Tatu. Kwa hiyo, vijiji vyote Mheshimiwa Silinde katika Jimbo lako la Momba vitapatwa umeme wa uhakika kupitia Mradi wa REA Awamu ya Tatu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa muda wetu unakwenda na leo tuna Muswada ambao lazima uishe leo, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Masoud.

Na. 58

### **Kuboresha Sekta ya Uvuvi Nchini**

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM** aliuliza:-

Uvuvi ni miongoni mwa sekta inayochangia Pato la Taifa, lakini Serikali imekuwa na kigugumizi cha kuboresha sekta hii wakati tukielekea katika Tanzania ya viwanda na uchumi wa kati.

Je, Serikali ina mkakati gani madhubuti wa kuboresha sekta ya uvuvi nchini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kutengeneza zana za uvuvi. Hadi sasa jumla ya viwanda vitatu vya kutengeneza boti aina ya *fibre glass* na viwanda viwili vya kutengeneza nyavu vimeanzishwa. Aidha, viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi 48 vinavyojumuisha viwanda vikubwa 15 na vidogo 33 pamoja na maghala ya kuhifadhi mazao ya uvuvi 38 yameanzishwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Sambamba na hilo Serikali ikishirikiana na sekta binafsi inafanya juhudi ya kutafuta wawekezaji wa kujenga viwanda vya kuchakata samaki aina ya jodari katika huu Ukanda wa Pwani wa Bahari ya Hindi, hili likifanikiwa litawezesha wavuvi kuongeza thamani ya mazao ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imedhamiria kuongeza uzalishaji wa Samaki kupitia ufugaji wa samaki (*aquaculture*) kutoka metriki tani 10,000 mpaka metriki tani 50,000 ifikapo mwaka 2020. Aidha, Serikali ina dhamira ya kuanzisha vituo vipya vitatu na kuboresha vituo vingine 15 vya uzalishaji wa mbegu bora za samaki, kushirikisha sekta binafsi na taasisi za kitafiti katika kuboresha teknolojia na uzalishaji wa mbegu na chakula bora cha samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua zake za kuendeleza uvuvi wa bahari kuu, Serikali imekamilisha mazungumzo kati yake na Mamlaka ya Bandari ya Dar es Salaam ambapo gati namba sita litatumwa na meli zinazovua katika ukanda wa uchumi wa bahari, ili kushusha samaki. Aidha, juhudi za ujenzi wa bandari ya uvuvi zinaendelea ambapo tayari mtaalam elekezi wa kufanya upembuzi yakinifu amepatikana.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza nina masikitiko kwamba majibu ambayo ametoa Mheshimiwa Waziri, ama wataalam wake hawajui sekta ya uvuvi na wanaelekea zaidi kwenye shughuli za mifugo au itakuwa kuna danadana za hapa na pale. Nina maswali mawili ya nyongeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia mkakati wa Tanzania ya viwanda na uchumi wa kati, Serikali imekuja na majibu wanasema wanataka kuanzisha viwanda vitatu vya kutengeneza boti aina ya *fibre glass*. Tanzania ya viwanda

kuelekea uchumi wa kati wanataka kutengeneza boti sasa ndogo (*fibre glass*), Serikali ituambie ina mkakati gani wa kuweza kununua meli za uvuvi za kisasa kwenda kwenye bahari kuu ambapo watawua samaki ambao wanavuliwa na nchi nyingine? Hiyo, tunataka mkakati wa ziada, sio mnasema mnataka kununua *fibre glass*? *Fibre glass* kwenye uchumi wa kati, Tanzania ya viwanda? Maajabu makubwa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, wanasema Serikali kwamba sekta ya uvuvi hii wanataka kuboresha maisha ya wavuvi, wametenga wana shilingi milioni 400 kwa ajili ya kuboresha ruzuku za uvuvi na mambo mengine. Shilingi milioni 400 Mheshimiwa! Wavuvi ni maskini, shilingi milioni 400 ndio kitu gani? Kwenye bahari na kwenye maziwa? Serikali ituambie mna mkakati gani wa ziada kuboresha maisha ya wavuvi hasa wadogo wadogo sio shilingi milioni 400. Ndio Tanzania ya viwanda kuelekea uchumi wa kati hiyo? Tupe majibu ya uhakika, Serikali inasemaje juu ya kuboresha maisha ya wavuvi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Masoud kama ifuatavyo:-

Kuhusu uwekezaji wa ununuzi wa meli kwa ajili ya uvuvi katika bahari kuu nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali yenyewe haina nia ya kununua meli, lakini kinachofanywa ni kuweka mazingira wezeshi na kuhamasisha sekta binafsi iweze kuwekeza katika ununuzi wa meli pamoja na uvuvi katika bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shilingi milioni 400, nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba hiyo ni sehemu ndogo tu....

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaomba utulivu ndani ya Bunge tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** ...shilingi milioni 400 zilizotolewa kwa ajili ya kuwawezesha wavuvi ni sehemu ndogo tu ya jitihada mbalimbali zinachokuliwa na Serikali kwa ajili ya kuendeleza sekta ya uvuvi.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kwa kunipa nafasi. Wakazi wa Wilaya ya Nkasi karibu nusu wanakaa mwambao wa Ziwa Tanganyika ambapo wanajishughulisha na shughuli ya uvuvi. Serikali kupitia Mkuu wa Mkoa imepiga marufuku kabisa shughuli za uvuvi kufanyika



mchana na kufanyika kwa kutumia vifaa vyovyote vya kielektroniki kama vile tochi na taa za solar ambazo zinatoa mwanga mdogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa wavuvi wamekaa na wamechanganyikiwa hakuna kazi yeyote wanayoifanya na hawawezi kuendesha maisha yao kwa sasa hivi. Kwa hiyo, naiomba Serikali ione namna ambavyo wataiona changamoto hii kwa namna ya pekee kwa sababu wananchi hawana namna ya kujisaidia kwa sasa. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kama alivyosema kwamba katika siku za karibuni kumetokea hali ya sintofahamu kwa wavuvi wa Ziwa Tanganyika kutokana na katazo ambalo limefanywa na Serikali. Wabunge wanaotoka katika ukanda huo wengi wamekuwa wakija ofisini kwetu kufuatilia akiwepo Mheshimiwa Keissy, yeye nimeongea naye sana kuhusu hili.

Nimhakikishie tu kwamba kilichotokea ni mkanganyiko kidogo kuhusu kanuni ambayo hairuhusu uvuvi kwa kutumia jenereta na kwa kutumia solar ya zaidi ya wati 50; maelekezo sahihi tumeshayatoka kwa hiyo tunaamini katika siku chache hili litakuwa limeshakamilika na wavuvi wataendelea kuvua kama kawaida.

Na. 59

### **Athari kwa Wakulima wa Pamba**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA (K.n.y MHE. DOTTO M. BITEKO)** aliuliza:-

Wakulima wa pamba Wilaya ya Bukombe na Geita kwa jumla katika msimu wa mwaka 2015 walipatiwa mbegu na dawa yasiyokuwa na ubora ambayo hayakuuwa wadudu.

Je, Serikali inawaambia nini wakulima walioathirika na pembejeo hizo na inachukua hatua gani kuhakikisha jambo hili halijirudii tena?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dotto Mashaka Biteko, Mbunge wa Bukombe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepata taarifa kuhusu tatizo lililowapata wakulima wa pamba katika maeneo mbalimbali ikiwemo wale ikiwemo wale wa Mkoa wa Geita kwa kusambaziwa mbegu ambazo hazikuwa na ubora

unaotakiwa. Aidha, katika msimu wa kilimo wa mwaka 2015/2016, viuatilifu vilivyosambazwa kwa wakulima vilishindwa kudhibiti wadudu wa pamba kikamilifu katika maeneo mengi ikiwemo Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ununuzi wa pembejeo za zao la pamba unaratibiwa na Mfuko wa Kuendeleza Zao la Pamba (CDTF), usambazaji wa pembejeo hizo baada ya ununuzi unaishirikisha Bodi ya Pamba. Kufuatia taarifa za uwepo wa pembejeo hafifu hususan viatilifu Serikali iliagiza TPRI kufanya uchunguzi wa malalamiko ya wakulima. Uchunguzi ulibaini kwamba kiuatilifu kinachofahamika kwa jina la *Ninja 5EC* ndicho kilichokuwa kinalalamikiwa na wakulima kwa utendaji hafifu. Uchunguzi zaidi ulionesha kwamba baadhi ya sumpuli za kiuatilifu hicho zilikuwa na kiwango kidogo cha kiambato amalifu (*active ingredient*) ya kinachotakiwa, hivyo, kiuatilifu hicho hakingeweza kuwa wadudu waliolengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za uchunguzi uliofanywa na TPRI, Bodi ya Pamba, CDTF, wawakilishi wa wasambazaji, wakulima na wadau wengine zimeonesha kwamba viuatilifu hivyo vya *Ninja 5EC (Batch Na 2014102001 na KR4003)* vilinunuliwa kutoka Kampuni ya *Positive International Limited* na kusambazwa na UMWAPA na kutoka Kampuni ya *Mukpar Kagera Limited (Batch Na. KR1400451103)* na kusambazwa na Mfuko wa Kuendeleza zao la Pamba. Aidha, uchunguzi unaonesha kwamba kuna *batches* za viuatilifu za mwaka 2014/2015 zilisambazwa pia, ambazo inawezekana kama hazikutunzwa vema ubora ungeweza kuwa na mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba matumizi ya kiutalifu hafifu kwa mujibu wa uchunguzi huu kilikuwa na athari kwa wakulima. Kufuatia taarifa hizo za uchunguzi Serikali inakamilisha taratibu za kuchukua hatua za kisheria kwa wale wote waliyohusika na kadhia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia changamoto za utoaji wa mbegu za pamba ambazo unatokea, Serikali katika msimu wa mwaka 2016/2017 iliamua kufanya majaribio ya utoaji wa mbegu za pamba ambazo zimekuwa zikisambazwa hapo awali bila kujua ufanisi katika utoaji wake. Matokeo ya majaribio ya utoaji yamewezesha kutoa maelekezo kuhusu *batches* za mbegu za pamba zenye sifa za msingi kusambazwa kwa wakulima katika msimu wa kilimo wa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha jambo hili halijirudii tena, Serikali itaanza kuzalisha mbegu bora za pamba za *UKM08* katika mashamba maalum ili hatimaye baada misimu miwili ya kilimo wakulima wote waweze kupata mbegu bora za pamba.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa Mkoa wa Geita, hususan Jimbo la Bukombe mwaka wa jana walivyogawiwa mbegu na pembejeo mbegu zile hazikuota, na waliahidiwa kupewa fidia, hawakupewa na sasa wanaogawa mbegu ni wale wale waliowatia hasara mwaka jana. Je, Serikali inawahakikishiaje wale wananchi, kama zile mbegu hazitaota ni nani ataingia gharama ya kuwafidia?

Swali la pili, asilimia kubwa ya Jimbo la Geita vijijini linategemea sana uvuvi. Kumekuwa na *operation* nyingi sana za kukamata wavuvi na mitego midogo midogo, na kuchoma mitego yao kwa Wakuu wa Wilaya.

Je, Serikali inafanya *operation* lini kwenye viwanda vinavyotengeneza, vinafahamika na makontena yanayoingia, badala ya kwenda kuwasumbua wale wavuvi maskini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi. Mheshimiwa Waziri muhusika.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika misimu miwili ya nyuma mfululizo kuna baadhi ya mbegu ambazo ziligawanywa na Mfuko wa Kuendeleza Zao la Pamba kupitia *gineries* mbalimbali ambazo hazikuota na hasa mbegu ambazo hazikuota ni zile ambazo zilikuwa zimenyonyolewa nyuzi. Utaratibu ulifanyika wa kujua ni nani aliyekuwa amefanya kosa kwa sababu *batch* hizo hizo kuna maeneo ziliota vizuri na kuna maeneo mengine hazikuota vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wataalam waliingia katika kutafiti ni kutu gani kimesababisha mbegu ambazo zimezalishwa sehemu moja, maeneo mengine sziote na maeneo mengine ziote. Ziko sababu mbalimbali, zingine zikiwemo za upandaji usiokuwa sahihi wa mbegu hizo, lakini ziko pia mbegu ambazo zilibainika kwamba wakati zinanyonyolewa wauzaji wa hiyo pamba walikuwa wamezimwagia maji ili kuongeza uzito wa pamba yao, kudanganya katika ununuzi na hivyo kuzifanya zipoteze ubora hata wakati zinanyonyolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni *complex* ili kujua ukweli kwamba kosa ni la msambazaji au ni la aliyezinyonyoa au ni la mkulima aliyeuza mbegu ambayo ilikuwa imemwagiwa maji. Tutakapokuwa tumejiridhisha *exactly* nani aliyefanya jambo hilo ni nani, huyo ndiye tutakaye mchukulia hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *operations* zinazoendelea nchi nzima kwenye uvuvi, kwanza hili swali siyo mahali pake, lakini nitalijibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi haramu tutaushambulia na kupigana nao vita popote utakapojitokeza na kwa namna zote. Kwa hiyo, hatukomei katika kukamata wavuvi wenye nyavu, isipokuwa tunakwenda kwa wazalishaji, wasambazaji na waingizaji wa hizo zana haramu nchini. Ndiyo maana umeona tumekamata viwanda wanazalisha nyavu haramu, malori ya wanaosafirisha, tumeingia kwenye maduka mahali zinakouzwa na tunawakamata wavuvi wenyewe wanaotumia hizo zana haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kwenda hatua zaidi, kwamba sasa tunaanzisha utaratibu wa kwenda na mashua huko huko ziwani, tutawahukumu huko huko, wale tutakaowakuta wanatumia zana haramu. Na humu barabarani kama agizo lilivyo la Mkuu wa nchi, tukikukamta hata wewe una malori tunakushitaki na ku-*confiscate* kila kitu ulichonacho.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, napenda tu kuuliza swali dogo kwa Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa Bodi ya Pamba muda mwingi iko Dar es Salaam na Makao Makuu yako Dar es Salaam, na kwa kuwa Mkoa wa Simiyu ndio Mkoa unaoongoza kulima pamba hapa nchini. Je, Serikali inatoa tamko gani kwa wakulima ambao wamekuwa wakipata mbegu hizi na dawa ambazo hazivasaidii na wala hawapewi fidia. Ni lini Bodi hii itahamia karibu na Mikoa ambayo inazalisha pamba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi ameshatoa agizo la Bodi ya Pamba kuhamia Mwanza na kwa taarifa tulizonazo ni kwamba wanatakiwa wawe wamehama kabla ya tarehe 10 mwezi huu.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jinsi Mheshimiwa Waziri alivyojibu swali lake, kwamba bado hawajagundua nani ambaye amesababisha tatizo, lakini Serikali iliji-*commit* kulipa fidia. Sisi tunaotoka Kanda ya Ziwa suala la pamba limekuwa ni *issue* kubwa sana.

Je, Mheshimiwa Waziri, tatizo la pamba likijitokeza tena, uko tayari kujuzulu kwa sababu majibu yako tayari unajikanganya hapa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri kama ofisi inawezekana anavyosema Mheshimiwa Mbunge alitoa majibu ya kusema Serikali italipa fidia. Lakini hizo fedha ni fedha ya umma ambayo haiwezi ikalipwa tu bila kujiridhisha kwa kweli kwamba anayelipwa anastahili na kwamba Serikali inayo *liability* katika hilo jambo. Kwa hiyo, ni lazima kuwa na uhakika kwamba kwanza kweli Serikali inayo *liability* katika hilo jambo, lakini pili anayelipwa anastahili kulipwa hizo fedha na ndiyo maana hatua hizi zinafanyika. Kama nilivyosema kwenye suala la viuatilifu, tumekwisha jiridhisha *beyond doubt* nani wamehusika na hilo kosa la kusababisha dawa zisiwe na *effect* katika kuua wadudu kama ilivyotarajiwa na kwa hiyo hawa watachukuliwa hatua kama sheria inavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hata kwenye mbegu, tutakapajiridhisha *exactly* ni nani muhusika kwanza hawa watachukuliwa hatua na kama ni Serikali, itakuwa na wajibu wa kulipa tutafanya namna hiyo.

Na. 60

### **Hitaji la Chuo cha Ufundi Stadi Nkasi**

**MHE. ALLY M. KEISSY** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais alipokuwa Wizara wa Ujenzi wakati wa Awamu ya Nne aliahidi kwamba baada ya barabara ya Sumbawanga - Mpanda kukamilika kwa lami majengo yaliyopo katika kijiji cha Paramawe, Wilayani Nkasi yatatumika kwa ujenzi wa VETA, hasa ikizingatiwa kuwa Wilaya ya Nkasi haina chuo hicho.

(a) Je, Serikali iko tayari kutumia majengo hayo kwa ajili ya chuo cha VETA?

(b) Je, Serikali, iko tayari kwenda kuyaona majengo hayo mara barabara itakapokamilika?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, (a) napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ipo tayari kutumia majengo yaliyopo katika kijiji cha Paramawe, Wilayani Nkasi ambayo ni kambi ya ujenzi wa barabara ya lami ya Sumbawanga - Mpanda kwa ajili ya Chuo cha Ufundi Stadi chini ya Mamlaka

ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (VETA) ili kuweza kutoa mafunzo ya ufundi stadi baada ya kukamilika kwa ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, (b), Serikali pia ipo tayari kutuma wataalam kutoka wa VETA kutoka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, kwenda kuyaona majengo hayo mara barabara hiyo itakapokamilika kwa lengo la kufanya tathimini na kujiridhisha juu ya ubora wake kwa ajili ya kutoa mafunzo ya ufundi stadi. Hata hivyo, majengo hayo tatatumika kutolea mafunzo ya ufundi stadi baada ya kukamilika kwa taratibu za kupata idhini kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni wamiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri kwa wananchi wa Wilaya ya Nkasi waendeleo kutumia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Chala, kuwapatia ujuzi vijana wakati juhudi za Serikali, za kuwatafutia chuo cha ufundi zikiendelea.

**MHE. ALLY M. KEISSY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa mara ya kwanza Serikali kutoa jibu zuri la kuridhisha kwa wananchi wa Nkasi.

Kwa kuwa aliyekuwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Pombe Magufuli aliniahidi mimi humu Bungeni kwamba mara baada ya kukamilika ile barabara yuko tayari kutoa yale majengo kwa Chuo cha Ufundi VETA. Na sasa barabara yetu inakwenda *speed* ya ajabu, imebaki kilometa 10 au 12 na wakandarasi wameniahidi Januari au Disemba kipande cha barabara hiyo kitakamilika.

Je, lini sasa mazungumzo kati ya Wizara ya Elimu na Wizara ya Ujenzi yataanza haraka iwezekanavyo wananchi wapate kile chuo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wake tumeupokea, na mara baada ya kumaliza Bunge hili, tutawasiliana na wenzetu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ili tuweze kuona suala hili kabla hata barabara hazijaisha.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Karatu, kuna majengo ambayo yalikuwa yanatumika na Halmashauri ya Karatu, na sasa Halmashauri imehamia kwenye majengo mapya na huku nyuma kulishakuwa na azimio la Baraza la Madiwani kwamba majengo yale yatumike kama Chuo cha VETA.

Je, Serikali iko tayari sasa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Karatu kutumia yale majengo ya zamani ili kuweza kufungua chuo cha ufundi VETA?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, nilipokuwa najibu swali la Mheshimiwa Keissy nilijibu kwa *confidence* kwa sababu majengo hayo ninayafahamu, nikiwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa na mimi mwenyewe pia nilishiriki kuona kwamba yangefaa kutumika hivyo. Sasa katika hili ambalo umenifahamisha kuhusu majengo ya Karatu, naomba tuweze kuyaangalia kwanza kabla sijatoa majibu. Kwa hiyo, tutafanya utaratibu wa kuja kuyaona.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa yalikuwepo makubaliano kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Bahi na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi miaka minne iliyopita ya kufungua Chuo cha VETA katika Wilaya ya Bahi, katika kijiji cha Kigwe na yako majengo yaliyokuwa ya Chuo cha Kilimo ya Halmashauri na Wizara iliomba ipewe majengo yale ili iweze kufungua chuo cha VETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Bahi kupitia kikao cha Madiwani miaka mne iliyopia iliyakabidhi majengo yale kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, na Naibu Waziri wakati huo Mheshimiwa Mulugo alikwenda kutembelea majengo yale na akayakubali kwamba yanafaa kufunguliwa Chuo cha VETA. Lakini hadi sasa miaka mne imepita majengo yale yamekaa bure, Wizara haijarudi tena.

Je, ni lini sasa Wizara itarudi pale kuendelea na mchakato wake wa kufungua chuo cha VETA katika Halmashauri ya Bahi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu kwa pamoja kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao wanaona kuna majengo yanayostahili kuweza kutumika kama sehemu za kuweza kutolea mafunzo ya ufundi, wanipe taarifa hizo ili tuweze kuyatathimini kwa pamoja na hivyo kuwezesha sisi kupanua wigo wa kuongeza vyuo vya kutolea mafunzo ya ufundi katika nchi yetu, ikizingatiwa kwamba hata hivyo uhitaji ni mkubwa lakini imekuwani ngumu kwetu kuweza kujenga VETA kwa Wilaya zote kwa wakati mmoja.

Na. 61

## **Ujenzi wa Barabara Inayounganisha Mkoa wa Mbeya na Njombe**

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE** aliuliza:-

Halmashauri ya Busokelo ina changamoto za miundombinu ya barabara ambayo hairidhishi, na ukizingatia kuwa wananchi wake wanategemea zaidi shughuli za kilimo na usafirishaji wa gesi asilia ya *carbondioxide*.

(a) Je, ni lini Serikali itajenga barabara inayounganisha Mkoa wa Mbeya na Njombe kupitia Mwakaleli, kata za Kandete na Luteba?

(b) Je, ni lini Serikali itajenga barabara inayounganisha Jimbo la Busekelo (kijiji cha Kilimansanga) na Jimbo la Rungwe (kijiji cha Suma)?

(c) Vyanzo vya Halmashauri haviwezi kujenga barabara zote na hivyo kulazimika kuomba msaada *TANROADS*; je, ni lini maombi ya Halmashauri ya Busekelo, kuhusu kupandishwa hadhi ya barabara zaidi ya tano tulizoomba ili ziwe chini ya *TANROADS* yatajibiwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Jimbo la Busokelo lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara inayounganisha Mkoa wa Mbeya na Njombe kupitia Mwakaleli, kata ya Kandete na Luteba inapitia Katumba – Lusanje – Kandete – Ikubo hadi Luteba. Sehemu ya barabara ya Katumba - Lusanje – Kandete – Ikuba ambayo ni kilometa 34 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na *TANROADS*, na sehemu ya Ikuba hadi Luteba inahudumiwa na Halmashauri ya Busokelo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TANROADS* inaendelea kufanyia matengenezo kwa kiwango cha changarawe ili iendelee kupitika ambapo katika mwaka wa fedha 2016/2017 zimetengwa shilingi milioni 271.805 kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Katumba - Lwangwa hadi Mbambo na shilingi milioni 38.086 zimetengewa kwa ajili ya barabara ya Lusanje - Kandete hadi Ikubo. Mpango wa Serikali kwa sasa ni kuendelea kuzifanyia matengenezo barabara hizi ili zipitike wakati wote wa mwaka.



Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na milima yenye miinuko mikali kwa sasa hakuna barabara inayounganisha Jimbo la Busokelo na Jimbo la Rungwe kupitia vijiji vya Kilimansanga na Suma. Serikali haifikirii kufungua barabara ya kuunganisha maeneo hayo kutokana na milima hiyo mikali, hivyo barabara zilizopo tunaomba ziendelee kutumika kuhudumia maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, maombi ya Halmashauri ya Busokelo kuhusu kupandishwa hadhi barabara zaidi ya tano zilizoombwa ili ziwe chini ya TANROADS yanafanyiwa uchambuzi pamoja na maombi mengine yaliyopokelewa kutoka nchi nzima kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa kwenye Sheria ya Barabara Namba 13 ya mwaka 2007 na Kanuni za Menejimenti ya Barabara za mwaka 2009. Mara taratibu za uchambuzi zikikamilika barabara ambazo zina kipaumbele kiuchumi na kijamii zitapandishwa madaraja kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kwa masikitiko makubwa sana na nisononeke moyoni mwangu kwamba Mheshimiwa Waziri majibu aliyoleta hapa sio niliyouliza kwenye swali langu la msingi. Nimeuliza, barabara itajengwa lini ya Mkoa wa Mbeya na Njombe yeye amenitajia barabara za Katumba – Lusanje – Kandete. Nilikuwa namaanisha barabara inayotoka Mwakaleli kwenda mpaka Makete halafu iunganishwe na Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi swali la pili nimeuliza Jimbo la Busokelo litaunganishwa na Jimbo la Rungwe. Lakini Waziri anasema Serikali haifikirii kufungua barabara kuunganisha maeneo hayo kutokana na milima mikali, hivyo barabara ziendelee kutumika zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisikitike kwa sababu wananchi wa Jimbo la Busokelo katika Vijiji nilivyovitamka Suma pamoja na Kilimansanga ni zaidi 5,000. Akisema kwamba waendelee kutumia barabara hizo hizo wakati tayari hakuna muunganisho wa hizo barabara nashindwa kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili swali ningeomba liweze kujibiwa kwa mara nyingine tena kwa sababu majibu aliyojibu hapa sio, hayaniridhishi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimsihi Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kumaliza Bunge hili mimi nitakuwa na ziara eneo hilo. Kwa sababu katika jibu la msingi barabara anayoongelea ya Mkoa wa Mbeya kuunganisha na Njombe tumesema inapitia Mwakaleli, Kata ya Kandete na Luteba; na tumesema inapitia Katumba - Lusanje - Kandete - Ikubo hadi Luteba. Maadam anasema narudia yale yale, sasa kama nilichokisema anasema sio sahihi, naomba

tukakutane *site* ili tuweze kupata uhakika wa kile ambacho yeye anakiamini wakati sisi hiyo ndio tunavyofahamu.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa tatizo la Busokelo linalingana kabisa na Korogwe Vijijini. Kwanza nianza kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri wanayonifanyia kule Korogwe kwa kujenga daraja la Magoma. Barabara ya kutoka *Old Korogwe* kwenda Maguzoni ni barabara ya Mkoa, lakini daraja lake lilibomoka toka mwanzo wa mwaka huu.

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kujenga daraja hili ili wananchi waliokuwa wapo kwenye kisiwa waitumie barabara yao?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa daraja hilo tutalishughulikia na kwa nafasi hii nawataka *TANROADS* Mkoa wa Tanga walete taarifa kamili ya lini wamepanga kukifanya ili tuweze kutekeleza kile ambacho Mheshimiwa Mbunge na ambacho wananchi wa Korogwe wanakitaka. *(Makofi)*

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kama ilivyo kwenye Jimbo la Busokelo kuna barabara ya Mbalizi kwenda Makongorosi ambayo inapitia kwenye Bonde la Ziwa Rukwa ambayo tumegundua neema ya gesi nyingi sana. Sasa ni lini Serikali itajenga barabara hiyo ya Mbalizi - Makongorosi kwa kiwango cha lami ambayo ni ya Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Songwe? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali tunaifahamu barabara hiyo na tuna mpango thabiti wa kujenga. Lakini kwanza tupo katika mchakato wa awali hapo utakapo kamilika tutamtafuta mkandarasi ili tuweze kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Mheshimiwa Waziri naomba nikuulize swali; barabara ya Mgakolongo kwenda Kigarama mpaka Mlango upembuzi ulishafanyika muda mrefu na wananchi wameshindwa kuendeleza maeneo yao kwasababu walishawekewa "X". Barabara hii ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Bilakwate kwa namna anavyofuatilia ujenzi wa barabara zote mbili zinazopita katika Jimbo lake; moja upande wa Kaskazini na nyingine Kusini n nikubaliane na yeye kwamba hii ya Kusini inapita katika maeneo makubwa, ingawa hapa hajayasema lakini ameyaongea katika Ofisi yangu. Naomba nimhakikishie kwamba fedha zimetengwa kwenye mwaka huu wa fedha wa mwaka 2016/2017; nimuhakikishie tutajenga kabla ya tarehe 30 Juni, 2017.

**MWENYEKITI:** Ahsante, swali namba 62 limetolewa na mhusika, swali namba 63 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Bura.

Na. 62

### **Vituo vya Kusimamia Mabasi ya Masafa Marefu**

*(Swali hili liliondolewa katika orodha ya maswali na muuliza swali Mhe. Seif K. S. Gulamali)*

Na. 63

### **Wanawake Walionufaika na Benki ya Wanawake-Dodoma**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Benki ya wanawake nchini ilianzishwa kwa nia ya kuwasaidia wanawake kupata mikopo kwa haraka na kwa riba nafuu.

Je, ni wanawake wangapi wameshanufaika na mikopo ya benki hiyo kwa Mkoa wa Dodoma?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) ilianzishwa mwaka 2009 katika misingi ya kujiendesha kibiashara ikiwa na jukumu mahsusi la kuwapatia wanawake mikopo yenye masharti nafuu na kwa haraka. Kimsingi benki hii inatoa huduma zake kwa wananchi wote bila ubaguzi na ndiyo

maana tunasema hii ni benki pekee kwa wote. Benki ya Wanawake kwa Mkoa wa Dodoma ilianza kutoa huduma zake Disemba, 2012 ikiwa na vituo vinne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Septemba, 2016 benki kwa Mkoa wa Dodoma ilikuwa jumla ya vituo 18. Walionufaika na mikopo katika Benki ya Wanawake katika Mkoa wa Dodoma ni watu 19,740 kwa kipindi cha kuanzia Disemba, 2012 hadi Septemba, 2016; mikopo hii ina thamani ya shilingi 6,231,891,236. Kati ya hao wanawake waliopata mikopo hiyo ni 16,676 yenye thamani ya shilingi 5,063,765,641 sawa na asilimia 81 ya mikopo yote na wanaume wakiwa 3,064 ambao wamepata mikopo yenye thamani ya shilingi 1,168,125,595 sawa na asilimia 19.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa lengo la Serikali la kuanzisha benki hii ni kuwasaidia wanawake wanyonge waliopo vijijini; na kwa kuwa masharti ya Benki ya Wanawake haina tofauti na masharti ya mabenki mengine; na kwa kuwa riba inayotozwa na benki hii pia haina tofauti na riba inayotozwa na mabenki mengine. Je, lengo la Serikali la kuanzisha benki hii kuwasaidia wanawake wanyonge limefikwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa wanawake wengi wao wapo vijijini na benki hii haijaweza kuwafikia wanawake hao wa Tanzania waliopo vijijini. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wanawake wengi wanyonge waliopo vijijini wanafikiwa na huduma ya benki hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, (a) swali lake linahusu riba ya benki hii kuwa sawa na riba inayotolewa na mabenki mengine. Majibu yetu ni kwamba mwezi Machi mwaka huu wakati tukisherehekea sherehe ya Siku ya Wanawake Duniani, Waziri wa Afya alitoa agizo tena kwenye mkutano wa hadhara kwa Mkurugenzi wa Benki hii kwasababu kipindi hicho hakukuwa na bodi, waweze kulishughulikia suala hilo, ili kutengeneza dirisha maalum ambalo litawafikia wanawake wa nchi hii na mikopo yenye riba nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa msimamo wetu ni kwamba bodi ambayo tayari Mheshimiwa Waziri ameionda inalishughulikia suala hilo na tutatoa majibu baada ya kupata mwongozo kutoka kwa bodi husika ni namna gani wametokeleza agizo la Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wanawake wa vijijini watafikiwa na benki hii lakini pia pamoja na benki nyingine lakini pia pamoja na schemes nyingine za kuwawezesha wanawake kujiendeleza katika shughuli mbalimbali

za kiuchumi. Na ndiyo maana kwenye Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015/2020 Serikali imeanzisha mpango wa kupeleka shilingi milioni 50 kwenye kila kijiji kwa ajili ya kuwafikia makundi mbalimbali ya kujijenga kiuchumi. Benki yetu itaendelea kushirikiana na benki nyingineza kijamii kama hizi *community banks* na benki nyingine kubwa ili kuweza kutoa mikopo kwa wanawake. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamoto, ujandae Mheshimiwa Sophia Mwakasaga.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Sophia Mwakagenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na nataka kujua *commitment* ya Serikali juu ya benki hii ya wanawake ni lini itaiongezea ruzuku ili hiyo riba ambayo imekuwa ni kubwa iweze kuwa ndogo kuweza kusaidia kuwakopesha wanawake hasa wa vijijini? (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *commitment* ya Serikali inajionesha wazi kwa Serikali kutenga bajeti ya shilingi bilioni moja kwenye mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kuiwezesha benki hii kufungua dirisha maalum kwa ajili ya mikopo kwa wanawake. Hiyo ndio *commitment* yetu tunasubiri utekelezaji tu. (Makofi)

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa walengwa ni wakina mama ambao wengi wao bado wako Vijijini kama muuliza swali alivyosema. Lakini ukiangalia riba wanatozwa ni sawa sawa na wafanyabiashara wa kawaida na wao wanategemea kilimo. Sasa je, benki hii ili wafikie akina mama wakulima walipo maeneo tofauti na kule Kilolo inaonaje sasa ikiwapa mkopo uwe wa muda mrefu badala ya kuwapa kama wafanyabiashara ndogo ndogo? (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la riba ni suala ambalo linazingatia masharti yanayotolewa na *regulator* ambaye ni Benki Kuu na kutokana na masharti hayo benki yetu haiwezi kukiuka masharti ambayo yanawekwa na Benki Kuu ili tu kuwafikia akina mama na ndiyo maana Waziri wa Afya aliagiza tutengeneze *scheme* maalum kwa ajili ya kuwafikia akina mama wa vijijini na akina mama wajasiriamali wadogo wadogo ili riba itakayotolewa na benki hii iwe ni mahususi na iwafikie akina mama hawa waweze kupata mikopo nafuu zaidi kuliko ilivyo sasa. Kwa hiyo, suala hili tunaliangalia. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi.

Na. 64

### **Matatizo Yaliyopo Katika Sekta ya Afya**

**MHE. SILAFU J. MAUFI** aliuliza:-

Wananchi wamehamasika kujenga zahanati kwenye vijiji vyao lakini baadhi hazijakamilika na hata zile zilizokamilika hazijafunguliwa bado na watumishi nao hawatoshenzi mahitaji; hali hii inasababisha hospitali za mkoa ambazo ndizo za rufaa kuwa na msongamano mkubwa wa wagonjwa hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya Wilaya hazina Hospitali za Wilaya.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani ya utekelezaji wa kutoa unafuu wa uchangiaji huduma kwa akina mama wajawazito wanaoenda katika Hospitali za Rufaa?

(b) Je, ni lini Serikali itachukulia afya kuwa ni kipaumbele cha nchi hasa ikizingatiwa kuwa afya ni kila kitu katika maisha ya mwanadamu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu (a); Sera ya Afya ya mwaka 2007 inaeleza kuwa huduma za akina mama wajawazito katika vituo vya ngazi zote ni bure na hazipaswi kuchangiwa. Aidha, mwongozo wa uchangiaji pia umesitiza utekelezaji wa sera hii. Ili kuhakikisha akina mama wajawazito wanapata huduma wanazozihitaji Wizara inahakikisha wanakuwa na vifaa muhimu vya kujifungulia, ambapo vifuko maalum vyenye vifaa vya kujifungulia (*delivery packs*) vitasambazwa kwa wanawake 500,000 nchi nzima kulingana na uhitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu (b); siku zote Serikali imekuwa ikiweka kipaumbele kwa sekta ya afya katika nyanja zote na ndiyo maana Serikali inatoa huduma ya afya bure kwa watu wasiojiweza na kwa usawa kwa wote. Sekta ya afya imeendelea kuwa ya kipaumbele kwa Serikali kwani katika mgao

wa bajeti ya mwaka 2016/2017 imekuwa ya tatu kwa kutengewa asilimia 9.2 ya bajeti yote.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri katika suala, hili ninapenda kuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vifaa hivyo anavyovizungumzia ambavyo vinasambazwa katika maeneo yetu ya zahanati, kwa Wilaya yetu ya Sumbawanga, Wilaya ya Nkasi, Wilaya ya Sumbawanga Vijijini pamoja na Kalambo vifaa hivi havipo. Kama vinasambazwa vinasambazwa lini? Na je, Serikali itachukua mpango upi mkakati wa kuweza kufuatilia na kuhakikisha kwamba vifaa hivi vimesambazwa katika maeneo yetu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwamba Mkoa wa Rukwa ni Mkoa uliopo pembezoni; ni Mkoa ambao hauna Hospitali za Wilaya. Hata juzi Mheshimiwa Malocha alizungumzia suala la Hospitali ya Wilaya, kwa maana ya kituo cha Rahela kipasishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado Mkoa wa Rukwa hauna Hospitali ya Wilaya, kwa hiyo ndio maana hospitali yetu ya Rufaa ya Rukwa inakuwa na msongamano wa wagonjwa wengi katika eneo lile.

Sasa ni lini Serikali itahakikisha zahanati zetu, vituo vyetu vya afya vinakuwa katika ukamilifu wake na vifaa tiba vyake ili kuondoa msongamano katika Hospitali yetu ya Mkoa wa Rukwa? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwamba vifaa vitasambazwa lini? Mpaka sasa tunavyozunguza, hatujaanza kuvisambaza vifaa hivi kwa sababu vifaa hivi 500,000 vinatokana na tamko alilolitoa Mheshimiwa Waziri wa Afya wakati wa bajeti kama mpango maalum. Bajeti imeanza kutekelezwa mwezi Julai na bado hatujapokea fedha kwa ajili ya kutekeleza mpango huu mzuri ambao Waziri wa Afya ameuangazisha kwa majaribio mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa ambavyo vinapaswa kuja kwa utaratibu wa kawaida vimeendelea kupelekwa kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini na hivi 500,000 ni kwa ajili tu ya kufanya majaribio ya kuona kama tukiwapa *delivery packs* akinamama wanaoenda kujifungua, pengine inaweza ikasaidia kupunguza changamoto mbalimbali zilizopo kwenye mfumo. Kwa hiyo, huu ni mpango mpya na maalum na bado haujaanza kutekelezwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na shaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuhusu Vituo vya Afya na Zahanati kuweza kutoa huduma kwenye Mkoa wa Rukwa; kwanza, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya Bunge hili, ziara yangu ya kwanza ni Mkoa wa Rukwa. Mwezi uliopita kabla ya bajeti hii ya Bunge hili nilifika kwenye Mkoa wa Katavi. Baada ya Bunge hili nitafika kwenye Mkoa wa Rukwa kuona ni namna gani tunaweza tukashirikiana nao kuwawezesha kuanzisha huduma za upasuaji na huduma za maabara kwenye vituo vyote vya afya vilivyopo kwenye mkoa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Hospitali za Wilaya, yeye kama Mbunge akishirikiana na Wabunge wa Majimbo, wanapaswa kukaa kwenye vikao vyao vya Halmashauri na kupanga mpango kabambe wa kujenga hospitali hizi na Serikali Kuu itawasaidia pale ambapo watakuwa wamekwama. Napenda watambue kwamba jukumu hili ni lao kama Halmashauri kuanzisha miradi ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya na sisi Serikali Kuu tunawajengea uwezo tu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Aysharose Matembe; na Mheshimiwa Koshuma ajiandae.

**MHE. AYSHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tatizo lililopo katika Mkoa wa Rukwa halina tofauti na tatizo lililopo katika Mkoa wa Singida.

Swali; je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Hospitali za Wilaya za Mkoa wa Singida na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida inapata vifaa tiba vya kutosha kama vitanda vya kujifungulia ili kuwasaidia wanawake wajawazito ambao hutumia muda mrefu wa kutembea kufuata huduma hizo za afya? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba Mheshimiwa Aysharose atambue kwamba, mimi kama daktari na kama baba wa wanawake na kama mume wa mwanamke, nina *passion* ya kipekee na mambo yote yanahusu wanawake na ndiyo maana nikapewa jina la Balozi wa Wanawake. Kwa msingi huo, toka nimeteuliwa kwenye nafasi hii, nimezunguka kwenye zaidi ya vituo 120 vinavyotoa huduma za afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara zangu nimekuwa nikihamasisha ujenzi wa *theatre* na maabara ambazo zitakwenda kuboresha huduma ya mama na mototo kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini. Hivyo, namhakikishia kwamba vifaa tiba ni sehemu muhimu ya mpango huu



ambao tumeuanzisha wa kuboresha huduma za upasuaji na huduma za akinamama wajawazito kwa ujumla wake. Kwa hiyo, Mkoa wa Singida nimeshafika mara mbili toka nimateuliwa na katika ziara zangu nimekuwa nikihamasisha mambo haya yatekelezwe na Halmashauri zenyewe, maana mpango huu siyo wa kwetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Koshuma; halafu Mheshimiwa Zakaria na Mheshimiwa Gekul wajiandae.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwa kuwa lengo la Serikali ni kutoa huduma za afya kwa mama wajawazito bure, hiyo ni nia nzuri; lakini katika Mkoa wa Mwanza, baadhi ya visiwa vimekosa huduma za afya kwa sababu ya ukosefu wa Vituo vya Afya pamoja na Zahanati; Visiwa hivi viko katika Wilaya ya Buchosa ambavyo ni visiwa vya Soswa, Nyamango, Chamagati, Gembale, Nayonzwa pamoja na Kata ya Buryaheke kule Wilayani Buchosa. *(Makofi)*

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba katika visiwa hivyo kunajengwa Vituo vya Afya ili kuwasaidia akinamama wajawazito wasitembee umbali wa zaidi ya kilometa 40 kupata huduma za afya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi. Wewe ni mtalaam, kwa hiyo, majibu yako yawe ya kitalaam.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mkakati wa kwanza, kila mwaka tunatenga fedha kwenye bajeti kwa ajili ya kuboresha huduma za akinamama wajawazito na watoto. Mkakati wa pili, tayari Serikali inafanya mkakati wa ku-optimize huduma zinazotolewa kwenye Vituo vya Afya, ndiyo huo niliouzungumza wakati nikijibu swali la Mheshimiwa Aysharose, kwamba tunahakikisha vituo vyote ambavyo vimesajaliwa kama Vituo vya Afya, vinatoa huduma *optimally*, yaani huduma za upasuaji na huduma za kimaabara kama ambavyo Sera ya Afya inaelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa tatu umetangazwa juzi na Mheshimiwa Waziri wa Afya wakati wa Mkutano wa *Global Financing Facility (GFF)*, ambapo tutajenga vituo 100 vipya vya afya na kufanya maboresho kwenye vituo hivyo kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma za akinamama wajawazito na watoto. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante! Ni zamu ya Mheshimiwa Gekul na Mheshimiwa Zakaria ajiandae.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa sababu ambazo Madaktari Wakuu au Waganga Wakuu wamekuwa wakitoa kwa suala zima la ukosefu wa dawa katika hospitali zetu ni kwamba, kundi hili la msamaha la wazee, akinamama wajawazito na watoto ni wengi na wanaugua mara kwa mara. Naomba nifahamu, Serikali mmefanya utafiti kwa kiasi gani ili kuona kwamba hili kundi halilemei makundi mengine na kusababisha ukosefu wa dawa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la wazee linapewa kipaumbele cha kipekee kwenye Serikali ya Awamu ya Tano, ndiyo maana kuna *portfolio* maalum ambayo iko chini ya Waziri wa Afya inayosimamia mambo yanayohusu maslahi ya wazee. Kwa msingi huo, huduma hizi za afya kwa wazee zimepewa kipaumbele na Waziri na ndiyo maana alipoteuliwa tu, alitangaza kwamba wazee wapewe dirisha lao maalum, lakini pia wazee wapate haki ya kutibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakoelekea, tumezielekeza Halmashauri zote nchini ziwakatie Bima ya Afya, aina ya CHF (Mfuko wa Afya ya Jamii), wazee wote waliopo kwenye Halmashauri zao ili wazee hawa badala ya kusema tu wanatibiwa bure, watibiwe kwa kutumia kadi zao za CHF.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa subiri. Samahani, Mheshimiwa Waziri utajibu pamoja na la Mheshimiwa Zacharia.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Wizara, mwezi Juni mwaka huu, 2016 katika Bunge hili nilitoa ushauri Serikalini kwamba pengine tungetenga fedha katika bajeti zetu ya kuhakikisha Kituo kimoja cha Afya kwa kila Halmashauri kinajengewa uwezo. Kwa mfano, katika Jimbo la Mbulu Mjini, wananchi wa Tarafa ya Nambisi wanatembea zaidi ya kilometa 25 kufuata huduma ambayo ni mahitaji zaidi ya Zahanati hadi Hospitali ya Wilaya. Je, Serikali itakuwa tayari kuupitia mpango huu upya na kuviwezesha Vituo vya Afya vya pembezoni kujengewa uwezo wa wataalam na vitendea kazi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, subiri kidogo kuna Mwenyekiti wangu wa Bajeti.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kwanza niulize swali linalohusiana na Halmashauri yangu ambayo inavyo Vituo vya Afya, cha Mahurunga na Kitere, ambavyo vinavyo vyumba vya upasuaji na vifaa vyote vinavyohitajika; lakini mpaka sasa hivi havijaweza kufanya kazi kwa sababu hakuna watalaam wa kuweza kufanya hizo huduma suala ambalo linakatisha tamaa kujenga vituo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika bajeti iliyopita tuliomba Serikali itenge pesa kupitia mafuta kwa ajili ya kujenga Zahanati na Vituo vya Afya, Serikali ikatuhidi kwamba tuipe muda ifanye tathmini nchi nzima ili kujua mahitaji halisi na kujua majengo mangapi hayajakamilika. Tulitaka kufahamu, je, Serikali sasa imeshakuwa tayari, imeshafanya hiyo tathmini ili iweze kuingizwa katika bajeti inayokuja? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, yote kwa mpigo. Nawe ni mtalaam vilevile. (Kicheko)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda kujibu maswali matatu; kwanza, la Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Hawa Ghasia la kuhusu Kituo chake cha Afya, ambacho kina kila kitu, lakini hakina watalaam; ana vituo viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, sekta ya afya ina upungufu wa watalaam takriban asilimia 48, lakini tayari Mheshimiwa Rais juzi amezungumza kwamba tutaajiri watalaam katika Sekta ya Afya, kwa hiyo, tutapanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunasubiri kuajiri watalaam, nitumie Bunge lako Tukufu kuwaelekeza Makatibu Tawala wa Mikoa wawapange upya watalaam walionao. Unaweza ukaenda katika Kituo cha Afya ukakuta kina watalaam 18, lakini kituo kimoja cha afya katika Wilaya hiyo hiyo kina watalaam watatu. Kwa hiyo, hili ni jukumu la Makatibu Tawala wa Mikoa kufanya *redistribution*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la Mheshimiwa Hawa Ghasia kwamba, je, ule mpango wa kufanya tathmini ya maboma ya Vituo vya Afya, tumefikia wapi? Ni kweli Wizara ya Afya pamoja na Ofisi ya Rais (TAMISEMI), baada ya kupitisha bajeti ya mwaka 2015, tulifanya tathmini na tumesha-*identify* kuna maboma mangapi ya Zahanati, kuna Vituo vya Afya vingapi ambavyo havijakamilika; na tayari Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango

yuko hapa, tumekubaliana badala ya kusema tunaenda kuvimaliza vyote katika mwaka mmoja, ndiyo narudi katika swali la Mheshimiwa Zacharia. Tuta-pick angalau Kituo cha Afya kimoja katika kila Halmashauri badala ya kusema tutafanya Kituo cha Afya katika kila Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mkakati wetu kila mwaka angalau Kituo cha Afya kimoja kwa kila Halmashauri baada ya miaka mitatu tutakuwa na Vituo vya Afya takriban 500, asilimia 100 zaidi ya Vituo vya Afya 500 ambavyo vimekuwepo nchini miaka 50 baada ya uhuru, sisi tutavipata katika kipindi cha miaka mitatu. Kwa hiyo, tutaleta katika bajeti ya mwakani hivyo, kituo kimoja cha afya kwa kila Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la Mheshimiwa Gekul, ni kweli hii sera ya msamaha kwa wajawazito, wazee na watoto chini ya miaka mitano, ndiyo mojawapo ya sababu ya changamoto katika upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba katika Vituo vya Afya vya Umma. Sasa ni takriban asilimia 60 kwa kweli ya watu ambao wanahudumiwa katika hospitali zetu za umma, ni hawa watu wa msamaha. Kwa hiyo, hawachangii wakati Sera ya Afya inasema, huduma za afya ni kuchangia. Mkakati wetu ni upi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema, nilitaka kuongeza, tunazungumzia *financing for the health sector*, jinsi gani tutatengeneza, jinsi gani tutagharamia Sekta ya Afya. Kwa hiyo, tunaenda kwenye Bima ya Afya kwa kila Mtanzania; maana yake, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuwakatia Bima ya Afya wanawake, wazee na watoto wa chini ya miaka mitano. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi wa Pili tutakuja kwako Bungeni, tulete mapendekezo yetu na tunategemea moja ya vyanzo vya fedha hizi ni zile kodi zinazotokana na mambo ya madhambi; *sin taxes*. Kwa mfano, pombe, sigara na bia na naamini Waziri wa Fedha na Mipango atatukubalia kwa ajili ya kufikia *Universal Health Coverage* itakapofika mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje, Mheshimiwa Maria Kangoye, kwa niaba yake Mheshimiwa Hawa Mchafu.

Na. 65

### **Viongozi wa Dini kupewa Heshima**

**MHE. HAWA M. CHAKOMA (K.n.y. MHE. MARIA N. KANGOYE)** aliuliza:-

Viongozi wa Dini wanaheshimika sana, wanahimiza utulivu na amani na kuliombea Taifa letu. Hata wakati wa kumwapisha Rais, Viongozi hawa hupewa nafasi ya kumwombea Rais na kuiombea nchi:-

(a) Je, ni lini Serikali itatoa umuhimu kwa Viongozi Wakuu wa kidini kupewa hadhi ya kupitia sehemu ya Viongozi wenye heshima (VIPs) katika viwanja vya ndege na sehemu ambazo kuna huduma kama hizo?

(b) Je, ni vigezo gani au utaratibu gani unaotumika kuwapa Hati za Kidiplomasia watu mbalimbali, lakini viongozi wetu wa kidini hawana hadhi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ndila Kangoye, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya Kumbi za Watu Mashuhuri, (VIPs Lounge) hasa katika viwanja vya ndege nchini, huratibiwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Utaratibu ni kuwa, Kiongozi wa Dini au mtu yeyote anayestahili kutumia sehemu hizo, hujaza fomu za kuomba kutumia na Wizara yangu imekuwa ikitoa vibali vya matumizi ya sehemu hizo pindi itokeapo maombi hayo ikiwa ni pamoja na Viongozi Wakuu wa Dini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa hati na nyaraka za kusafiria za aina zote hufanywa kwa kufuata Sheria Na. 20 ya mwaka 2002 ya Hati na Nyaraka za Kusafiria ijulikayo kama *Passports and Travel Documents Act, No. 20 of 2002*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 5 (1) cha Sheria hiyo, Mkurugenzi wa Uhamiaji ndio mwenye mamlaka ya kutoa hati zote za kusafiria. Hata hivyo, Kifungu cha 5 (2) (a) kinamruhusu Mkurugenzi wa Idara ya Uhamiaji kumpa uwezo, yaani ana- *delegate* kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuelekeza utoaji wa *pass* za kusafiria za kidiplomasia, (*power to authorize grant of diplomatic passport*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 10(3) cha Sheria tajwa kinaelekeza kuwa, wanaostahili kupewa Hati za Kidiplomasi wanapatikana katika jedwali Na. 3 katika Kifungu cha “ddd”, ambapo Mkurugenzi wa Uhamiaji amepewa mamlaka ya kutoa Pass ya Kidiplomasia kwa Viongozi Wakuu wa Taasisi za Kidini hapa nchini kwa kadri anavyoona inafaa. Hivyo, viongozi Wakuu wa Dini wamekuwa wakipewa Pass za kusafiria za Kidiplomasia kulingana na kipengele hicho hapo juu na kwa namna ambavyo mamlaka inayosimamia inavyoelekeza katika sheria husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa, Pass ya Kidiplomasia ni nyaraka maalum inayomwezesha mhusika kufanya kazi zake hasa za kidiplomasia.

Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine husika zinapitia upya Sheria hii ya Pass na Nyaraka za Kusafiria kwa lengo la kuifanyia marekebisho kwa kuangalia pia uzoefu wa nchi nyingine juu ya nyaraka hii muhimu. Pindi zoezi hili litakapokamilika, mapendekezo ya marekebisho hayo yatawasilishwa katika Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuridhiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mchafu.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake ya msingi amezungumzia juu ya kuleta sheria hii kufanyiwa marekebisho kwa kuzingatia uzoefu wa nchini nyingine juu ya nyara hii muhimu. Swali langu ni kwamba, je, ni lini sheria hii italetwa hapa Bungeni ili iweze kufanyiwa marekebisho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Serikali inachukua hatua gani ya kuwanyang'anya *Diplomatic Passport* watu ambao hawana tena sifa ya kuwa nazo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwamba ni lini sheria hii muhimu italetwa hapa Bungeni? Ni pale ambapo Taasisi husika zitakapomaliza kuirekebisha na kupitia process zote. Kwa sababu kuirekebisha inahitaji wadau wazungumze, wajadili na ipitie katika Wizara mbili husika na kuwatumia wadau ambao kwa namna moja au nyingine wanahusika moja kwa moja. Kwa hiyo, itakapokuwa tayari, italetwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la pili, kwamba tunachukua hatua gani kuwanyang'anya *passport* wale ambao hawastahili; pale ambapo wanapokuja kubadilisha zile *passport*, hawarudishiwi tena, wanapewa *passport*

ambazo ni za kawaida kutokana na sheria. Huo ndiyo utaratibu ambao unafanyika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa, tunakwenda Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Mheshimiwa Bilakwate.

Na. 66

### **Tatizo Kubwa la Maji - Kyerwa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Wananchi wengi katika Jimbo la Kyerwa wanakabiliwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa maji safi na salama, jambo linalorudisha nyuma shughuli za maendeleo:-

Je, ni lini Serikali itatumia maji ya Mto Kagera kuwapatia wananchi maji safi?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa muda mfupi, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 200 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika Miji ya Rubwera na Rwenkorongo ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya ya Kyerwa. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na ununuzi wa mabomba, uchimbaji wa mitaro na ulazaji wa bomba za kusambaza maji pamoja na viungo vyake; kukarabati tanki moja na ununuzi wa pampu mbili za kuvuta na kusukuma maji toka kwenye visima virefu viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa muda mrefu, kupitia Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imepanga kukamilisha mradi mkubwa wa maji kwa ajili ya Mji wa Kyerwa pamoja na vijiji vinavyozunguka. Taarifa ya upembuzi yakinifu itakapokamilika, ndipo tutawezesha kufanya maamuzi iwapo Mto Kagera ndiyo utumike kama chanzo au kama kuna vyanzo mbadala ambavyo vinaweza kutumika ambapo uzalishaji wa maji utakuwa wa gharama nafuu zaidi na endelevu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo la maji katika Jimbo la Kyerwa ni kubwa sana na wananchi wake hawapatii maji, hata asilimia 20 haifiki: Je, Serikali inawaahidi wananchi wa Jimbo la Kyerwa kama alivyojibu, “upembuzi yakinifu unaoendelea utakapokamilika mwaka 2017/2018;” Serikali inaahidi kutenga pesa ya kutosha kwa ajili ya kukamilisha mradi huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ili miradi hii iweze kusimamiwa vizuri, ni vizuri tukawa na wataalam. Wilaya yangu ya Kyerwa hatuna wataalam wa kutosha, lakini wataalam wenyewe hao waliopo hawana vitendea kazi kama gari na vifaa vingine. Je, Serikali ipo tayari kutuletea wataalam wa kutosha na vitendea kazi ili kazi isimamiwe vizuri? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi. Hili swali lina Wabunge wengi, lakini Waheshimiwa Wabunge, mnaona muda wetu umeshapita.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza alitaka kujua kama katika bajeti ya mwaka 2017/2018 tungeweza kuweka fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi huu ambao unaendelea kufanyiwa usanifu. Namwahidi kwamba kazi hiyo tutaifanya ili wananchi wetu kule waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la pili, kwamba Wilaya yake ina wataalam wachache; ni kweli wilaya nyingi hazina Wahandisi wala vifaa. Katika Program ya Sekta ya Maji Awamu ya Pili, tumeweka bajeti kwa ajili ya kununua magari na vifaa muhimu, lakini pia tumeomba vibali kwa ajili ya kuajiri Wahandisi wa kutosha ili tuweze kuwapeleka kwenye wilaya mbalimbali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ungando, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. ALLY S. UGANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia Mto Rufiji kutoa maji ili wananchi wa Kibiti, Bungu, Ikwiriri, Kimanzichana na Mbagala wafaidike na mto huo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.



**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ungando, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutumia Mto Rufiji au vyanzo vingine; haya tunafanya maamuzi baada ya kufanya usanifu wa maeneo yale tunayotaka kupeleka yale maji. Kwa hiyo, tunalinganisha gharama kwa wakati ule. Uwezo wa Serikali; kwa mfano, ukichukua maji kwenye mto na ukapeleka vijiji vingi au kilometa 100, gharama yake ni kubwa. Kwa hiyo, lazima uangalie uwezo pia wa Serikali. Kwa hiyo, kama kuna uwezekano wa kupata vyanzo ambavyo ni nafuu kwa gharama, tunaanza navyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango ya muda mrefu, tulishajibu hapa Bungeni kwamba tunafanya usanifu wa kuona uwezekano wa kuchukua maji ya Mto Rufiji na kuleta maeneo ya mpaka Mkuranga. Kwa hiyo, jambo hilo linafanyiwa kazi na Serikali. Muda utakapofika, basi tutawajulisha Waheshimiwa Wabunge kama hilo linawezekana kwa bajeti inayokuja au baada ya hapo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe na Mheshimiwa Massare jiandae. Wote muwe na maswali mafupi sana.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tatizo Kyerwa linafanana moja kwa moja na tatizo lililopo katika Halmashauri ya Wilaya Masasi. Tatizo letu kubwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ni masuala ya miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna maji ya kutosha. Serikali iliahidi kutenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuleta miundombinu itakayofikisha maji katika Vijiji vya Mbemba, Mbaju, Maparagwe pamoja na Chikunja. Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kupeleka pesa angalau kidogo kidogo katika hii miradi ili iweze kutekelezwa mara moja? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2016/2017, kila Halmashauri imetengewa fedha kwa ajili ya kuendeleza miradi ambayo ilishakuwa imeanza. Hii ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi. Fedha hizo hatutapeleka moja kwa moja; tumeagiza kwamba walete *certificate* kwa sababu nyingi wameshakuwa na Wakandarasi. Walete *certificate* ili tuweze kuwalipa wale Wakandarasi waweze kuendelea na utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Mheshimiwa Mbunge kuna Mkandarasi na kuna *certificate* ambayo haijalipwa, niletee ili tuweze kulipa, fedha zipo. Hatuwezi kupeleka fedha zikakae tu, tunataka fedha ziende na zifanye kazi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niulize swali dogo tu kwa kifupi. Kwa kuwa matatizo yaliyopo huko Kyerwa yanafanana sana na yaliyopo katika Jimbo langu la Manyoni Magharibi katika Mji wa Itigi ambao hauna maji kabisa toka nchi hii imepata uhuru. Je, sasa Serikali iko tayari kusaidiana na Halmashauri ya Itigi ili wananchi wa Itigi Mjini pale wapate maji? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu. Ni lini tu! Mjibu kwa kifupi sana. Mheshimiwa Maryam Msabaha, jiandae.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali imeahidi kupeleka maji katika Mji wa Itigi na mpango huo upo. Kwa hiyo, tunaendelea kufuatilia utekelezaji wa yale mambo ambayo tulishakubaliana kwa mwaka huu tunafanya nini. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, Serikali itahakikisha kwamba Mji wa Itigi unapata maji.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Maryam Msabaha. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha sasa tutatoa nafasi kwa wenye maswali tu.

Na. 67

### **Kazi za Vikosi vya Ulinzi na Usalama**

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA** aliuliza:-

Kazi za Vikosi vya Ulinzi na Usalama ni kulinda raia, mali zao pamoja na mipaka ya nchi, lakini kuna baadhi yao wanakwenda kinyume na sheria kwa kuwapiga wananchi na kuwasababishia ulemavu au vifo:-

(a) Je, mpaka sasa Serikali imeshawachukulia hatua gani?

(b) Je, mpaka sasa ni askari wangapi wamekutwa na hatia na kufukuzwa kazi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi hufanya kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Hata hivyo, kuna askari wachache ambao wamekuwa wakikiuka maadili na mwenendo mwema wa Jeshi la Polisi kama ambavyo imeainishwa katika Kanuni za Kudumu za Jeshi la Polisi, namba 103.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kinidhamu kwa watumishi wanaoonekana kwenda kinyume na maadili ya kazi za Jeshi la Polisi ikiwemo kuwapiga wananchi wasio na hatia. Mathalan, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2016 Juni, askari 200 walichukuliwa hatua za kinidhamu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya askari 152 walikutwa na hatia na kufukuzwa kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msabaha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Zanzibar kumekuwa na matukio ambayo yanaendeshwa na vikosi vya *Janjaweed*; na kama Kikosi cha Polisi mna taarifa hiyo, ni kwa nini kikosi hiki kimekuwa kikifanya matukio ya kuumiza wananchi na kuwasababishia ulemavu wa kuendelea na hata kutokujitafutia riziki kwa mahitaji yao ya kila siku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali kipindi cha uchaguzi kunakuwa na matukio mengi sana ya kupiga wananchi ambao hawana silaha na mnapambana nao na kuwaachia ulemavu wa kudumu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Maryam Msabaha anataka kujua kwamba kuna Kikundi cha *Janjaweed* ambacho kinapiga watu. Niseme tu kwamba kikundi cha *Janjaweed* mimi sikielewi. Ninachoweza kusema ni kwamba, kama Mheshimiwa Mbunge ana taarifa za kikundi chochote ambacho kinavunja sheria za nchi, basi ana wajibu wa kuhakikisha kwamba anashirikiana na nchi kufikisha taarifa hizo kwa Polisi ili hatua za kisheria zichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Polisi kupiga watu wakati wa uchaguzi, Polisi imefanya kazi kubwa sana kuhakikisha kwamba uchaguzi wetu unakwenda vizuri na sote ni mashahidi kwamba uchaguzi wa mwanzo na uchaguzi wa marudio Zanzibar ulikwenda kwa salama na amani na wananchi walitumia haki yao kidemokrasia vizuri kuchagua wale ambao wameamua wenyewe kuwachagua. Kwa hiyo, siyo sahihi kusema kwamba uchaguzi ulikwenda vibaya na Polisi wameshiriki katika kufanya uvunjifu wa sheria katika uchaguzi huo. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Swali linalofuata litaulizwa na Mheshimiwa Phillip Mulugo.

Na 68

### **Mahitaji ya Nyumba za Polisi – Songwe**

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga nyumba za Askari Polisi katika Wilaya mpya ya Songwe, hasa ikizingatiwa kuwa Maaskari wengi wameripoti ndani ya Wilaya hii mpya?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Phillip Augustino Mulugo, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua tatizo la makazi ya Askari Polisi katika Wilaya mpya ya Songwe na maeneo mengine nchini hususan kwenye mikoa mipya. Nia ya Serikali ni kutatua tatizo la upungufu wa makazi ya Askari Polisi kwa kujenga nyumba kwa awamu kupitia mpango wa ujenzi wa nyumba 4,136 nchi nzima. Mkoa wa Songwe ambao Wilaya ya Songwe inapatikana, ni sehemu ya mpango huo ambao utanza kutekelezwa baada ya utaratibu wa mikopo kukamilika. (Kicheko)

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiuliza Serikali maswali mawili tu ya nyongeza. Katika mpango wa Serikali wa kujenga nyumba 4,136, nataka tu kujua: je, Wilaya yangu ya Songwe ambayo ni wilaya mpya, itajengewa nyumba ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika mgao huo, ni pamoja na Askari Magareza pamoja na hawa Askari Polisi wa kawaida? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika majibu ya msingi ni kwamba Mkoa mpya wa Songwe ni moja katika mikoa ambayo itafaidika na awamu ya kwanza ya ujenzi wa nyumba 4,136.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kwamba Wilaya yake ya Songwe itahusika ama la, labda nichukue ili tuweze kulifanyia kazi, lakini ninachojua ni kwamba mkoa mzima utafaidika, kwa maana hiyo mgawanyo huu utafanyika kwa wilaya zote za mkoa mzima. Sasa kuhusiana na kiwango cha nyumba ngapi zitakwenda Wilaya ipi na ipi, takwimu hizo siwezi kumpatia kwa sasa hivi, lakini nitakapokuwa nimefanya utafiti, tutaweza kumjulisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kwamba je, katika suala hilo la ujenzi wa nyumba hizo Magereza wanahusikaje? Magereza wana mpango wao vile vile wa ujenzi wa nyumba ambao wao nyumba zao ni nyingi zaidi; zaidi ya nyumba 9,500 kama sikosei kwa ajili ya Magereza ambapo ni nyumba nyingi zaidi ya hizi za Polisi kwa nchi nzima. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza Naibu Waziri kwa majibu sahihi aliyoyatoa na pia nampongeza sana Mheshimiwa Mulugo kwa sababu amekuja mara nyingi sana ofisini kufuatilia jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mulugo, pamoja na mikoa yote mipya kwamba tutatoa kipaumbele kwa mikoa hiyo kwa sababu, licha ya makazi ya askari kutokuwepo, hata nyumba tu za kawaida za kupanga katika mikoa ile mipya na wilaya mpya ni kazi sana kwa Askari hao kupata tofauti na maeneo mengine. Kwa hiyo, tutalizingatia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja la faraja la kwanza, wakati tunaendelea kujadiliana, tutalifanyia kazi kwa umakini zaidi suala la *pango allowance* ambayo maaskari wetu wamekuwa wakipewa, kwanza kuwaondolea usumbufu.

Pili, kutengeneza utaratibu ambao utaendana na kiwango ambacho kina-*reflect* bei zaidi ya soko tofauti na sasa ambapo askari anapata asilimia 15 akiwa ngazi ya chini lakini hata akipanda, kiwango kile kinaendelea kuwa kilekile licha ya mshahara wake kupanda.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha. Nina matangazo. Tunaanza na wageni. Wageni waliopo Jukwaa la Spika: mgeni wa Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Job Ndugai ambaye ni Balozi wa Uingereza hapa nchini, Mheshimiwa Sarah Cooke.

*The High Commissioner of the United Kingdom, Sarah Cooke; it's a pleasure having you in Dodoma, welcome. Ameambatana na Maafisa wawili kutoka Ubalozi huo ambao ni Sylvester Ernest - Afisa wa Siasa Mwandamizi na Andrew Stephens - Mshauri wa Sheria za Jinai. (Makofi)*

Wageni wanne wa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, ambao ni wasaidizi wake kutoka Jimboni kwake Ruangwa, Mkoani Lindi. Ndugu Kasambe Hokororo, Ndugu Audiafast Ng'ombo, Ndugu Diones Malibiche na Ndugu Laurent Mmuya. (Makofi)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 53 wa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ambao ni kutoka vikundi viwili vya Kwaya ya Ushirika wa Ulemo, K.K.K.T. Dayosisi ya Kati, Jimbo la Ushora, Iramba Magharibi, Mkoani Singida pamoja na Kwaya ya K.K.K.T. Ipagala ya Mjini Dodoma, wakiongozwa na Mheshimiwa Samwely Shila - Diwani wa Kata ya Ulemo, Mheshimiwa Grace Matulu - Diwani wa Viti Maalum na Mchungaji Simon Mtawa kutoka Ipagala K.K.K.T. Karibuni. (Makofi)

Mgeni wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambaye ni rafiki yake kutoka Jiji la Dar es Salaam, Ndugu Peter Malya. Karibu Dodoma. (Makofi)

Mgeni wa Mheshimiwa Zainab Katimba ambaye ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Chamwino kilichopo Mjini Dodoma, Ndugu Joseph Seganje. (Makofi)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambao ni rafiki zake kutoka Jiji la Dar es Salaam, wakiongozwa na Sabina Kaphipa. Karibuni Dodoma. (Makofi)

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo: Wanafunzi 23 na Walimu watano kutoka Shule ya Sekondari ya Kiislamu ya Al-haramain kutoka Jiji la Dar es Salaam. Karibuni Dodoma. (Makofi)

Wanafunzi 45 wanaosomea fani ya Mazingira kutoka Chuo cha Madini kilichopo Mjini Dodoma. Wanafunzi wa Madini, karibuni sana. (Makofi)

Wanafunzi 18 na Walimu kutoka Chuo cha Biblia cha Kanisa la Evangelistic Assemblies of God Tanzania (EAGT) cha Mjini Dodoma, karibuni sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, anaomba kuwataarifu Wabunge kuwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ambao ndiyo unasimamia matibabu ya Waheshimiwa Wabunge, umeandaa utaratibu wa kupima afya kwa Wabunge kwa kushirikiana na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete iliyopo Muhimbili, Dar es Salaam.

Waheshimiwa Wabunge, huduma hii ya upimaji wa afya itafanyika kuanzia leo, tarehe 7 hadi tarehe 11, katika jengo la Zahanati ya Bunge. Mnaombwa kushiriki kwenye zoezi hilo muhimu la upimaji wa afya.

Tangazo la Semina. Naomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo saa 7.00 kutakuwa na semina kwa Wabunge wote kuhusu Ugonjwa wa Kifua Kikuu na maambukizo mseto ya Kifua Kikuu na UKIMWI katika Ukumbi wa Bunge Dodoma kuanzia saa 7.00 mchana.

Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club* anaomba kuwatangazia Wabunge matokeo ya mechi zilizochezwa jana. Mpira wa miguu Bunge Sports 1-1 Chato *Football Club*. Mpira wa pete Bunge queens 54 na Chato Queens 19. Bunge Queens katika mashindano mengine wamepata 64 na Msalato *Girls* wamepata 12. Waheshimiwa Wabunge, matangazo kama haya yaje siku kama ya jana, kulikuwa na matatizo huko Dar es Salaam msiambataniше na matokeo mengine ya Dodoma. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mwongozo Mheshimiwa Munde.

Subiri basi Shekhe!

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuongea kuhusu Mwongozo wa Spika.

Kwa kuwa, tumepata taarifa ya msiba wa Mzee wetu Mzee Samwel Sitta na kiukweli Taifa limepoteza Kiongozi mahiri, hususani watu wa Mkoa wa Tabora. Mzee Sitta alikuwa Mbunge kwa muda mrefu, alikuwa Spika wa Bunge hili kwa muda mrefu, lakini Mzee Sitta alikuwa Mwenyekiti wa Bunge la Katiba Bunge la Kihistoria. Kwa niaba ya Wabunge wenzangu na kwa unyenyekevu mkubwa naomba Bunge hili liweze kuahirishwa ili tuweze kupata muda wa kuomboleza na kutafakari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Nakubaliana na Mheshimiwa Munde, Msiba huu ni mkubwa umeligusa Taifa, umemgusa Mheshimiwa Rais, umegusa Watanzania, umeligusa na Bunge. Bunge limefanya kazi kubwa sana, Bunge limehudumia matibabu yote ya Mheshimiwa Marehemu, kwa heshima ambayo aliipa nchi yetu hii. Waheshimiwa Wabunge, lakini Bunge hili linaendesha na Kanuni na Kanuni zetu zinasema anapofariki Mbunge, Mheshimiwa Spika, alishastaafu kuwa Mbunge, kwa hiyo, naomba tuendelee mpaka hapo tutakapokuwa na maelekezo mengine. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

### KUHUSU UTARATIBU

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 152 na naomba niisome.

**MWENYEKITI:** Soma tena Kanuni.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 152, ndiyo hiyo ambayo umetoka kuitolea maelezo sasa hivi wakati unajibu hoja ya Mheshimiwa Munde, kwamba endapo Mbunge atafariki wakati Bunge likiwa katika shughuli zake Spika ataahirisha shughuli za Bunge kwa siku hiyo kwa ajili ya maombolezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni hii ilikuja kuwekwa kwenye Kanuni za Bunge baada ya *practice* ambayo ilikuwa imetokea kwa muda mrefu kwa Wabunge wanapofariki Bunge kuahirishwa na halikuwa kwenye Kanuni, baada ya kuona kwamba ni *practice* ndiyo likaingia kwenye Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka nchi yetu ipate uhuru tumekuwa na Maspika kadhaa, Maspika wote waliopoteza maisha wastaafu, walipoteza maisha Bunge likiwa halipo kwenye *session*. Mheshimiwa Adam Sapi Mkwawa alipoteza maisha Bunge halikuwa kwenye *session*, Mheshimiwa Erasto Mang'anya alipoteza maisha Bunge halikuwa kwenye *session*. Kwa hiyo, hakuna *precedent* yoyote ambayo tunaweza tukaitumia kwa ajili ya Mheshimiwa Samweli John Sitta.



Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kanuni ya 153 (2) inakupa wewe mamlaka ya kutengua Kanuni yoyote. Pili Bunge haliendeshwi kwa Kanuni peke yake, Bunge pia linaendeshwa kwa desturi na kwa maamuzi ya Maspika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, leo hii unaweza ukafanya maamuzi ambayo yatatusaidia huko baadaye kwa *precedent* zingine, kwa sababu tayari sasa tuna Maspika wastaafu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge hili liahirishe shughuli zake leo kwa ajili ya kumuenzi Mheshimiwa Samwel John Sitta na hoja iungwe mkono na iletwe hapa Bungeni iweze kuamuliwa kwa ajili ya kumuenzi Mzee wetu huyu ambaye ameitumikia nchi yetu kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto najua umeguswa na watu wote wameguswa, *ruling* yangu inabaki kama nilivyofanya maamuzi na mazishi ya Mheshimiwa Spika wetu mstaafu, mpendwa wetu aliyefariki yatagharamiwa kwa mujibu wa Kanuni za Viongozi wa Serikali.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu kuonesha kutokubaliana na maamuzi ya Kiti)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika,

**MWENYEKITI:** Katibu

**NDG. CHARLES MLOKA-KATIBU MEZANI:**

### **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2016 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments*) (No. 3) Bill, 2016)

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

*(Hapa Baadhi ya Wabunge walisimama kuashiria kutokubaliana na maamuzi ya Kiti)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Ester Bulaya, nasema tunakwenda kufanya shughuli za Bunge pamoja na hii. Mheshimiwa Zitto nakupa *last warning*, Mheshimiwa Zitto naomba Waheshimiwa nawaomba...

**MBUNGE FULANI:** Spika Mstaafu anakufa tunaendelea na Bunge?

**MWENYEKITI:** Nawaomba sana, Kiti kinaongozwa na Kanuni, Waheshimiwa nawaomba sana, kipindi hiki kigumu, Mheshimiwa Zitto nakuomba tumia taratibu za kuzungumza, nikisimama mimi wewe tulia.

**MBUNGE FULANI:** Tumia busara Mwenyekiti.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walisimama huku wakipiga makofi kuashiria kutokubaliana na maamuzi ya Kiti)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Ester Bulaya kaa chini, Waheshimiwa Wabunge najua namna mlivyoguswa na kila mtu ameguswa na mimi nafanya kazi kwa mujibu wa maelekezo ya Kanuni.

**WABUNGE FULANI:** Ahaaa!

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Subirini basi! Mbona mnaanza kiherehere? Nimeagizwa na mimi naletewa hapa maagizo kwa mujibu wa uzito wa suala lenyewe, Waheshimiwa Wabunge subirini, sasa niwaache ninyi msemi basi mimi nisiseme. Kamati ya Uongozi itakutana sasa wakati Bunge linaendelea.

Kamati ya Uongozi itakaa na kulipitia suala hili. Kamati ya Uongozi nendeni mkakae na mtuletee jibu baada ya dakika 10. Tuendeleo.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Kamati ya Uongozi iende, itujibu baada ya dakika 15. Mheshimiwa AG.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maadam nimepata fursa hii nichukue nafasi hii, kwa niaba ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ...

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Taarifa kwa AG.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bashe, tafadhali sana kaa

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bashe tafadhali sana kaa, Mheshimiwa AG endelea.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nichukue fursa hii kukupa pole wewe mwenyewe, kutokana na pigo kubwa la kuondokewa na Spika Mstaafu Mheshimiwa Samwel Sitta. Nichukue fursa hii pia kumpa pole mjane wa Mheshimiwa Sitta, Mheshimiwa Margaret Sitta na familia yake.

**MBUNGE FULANI:** Uwongo huo bwana hakuna pole.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2016, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 ya mwaka 2016 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments*) (No.3) Bill, 2016) Sasa usomwe kwa mara ya pili na Bunge lako Tukufu lijadili na hatimaye lipitisha Muswada huo kuwa sehemu ya Sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuwasilisha maudhui kuhusu Muswada huu, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kutujalia uhai na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kwa kutimiza mwaka mmoja katika Utumishi wa Umma kwa nafasi hiyo.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea  
bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa AG endelea.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kwa kutimiza mwaka mmoja katika Utumishi wa Umma kwa nafasi hiyo kama Mkuu wa Nchi ..

**MBUNGE FULANI:** Msiba, msiba,msiba!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu. Katika muda huo ameweza kutekeleza majukumu yake kwa

ufanisi mkubwa ipasavyo, namtakia kila la kheri katika utumishi wake kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Oya! Msiba

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuweza kuendesha ipasavyo Bunge letu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Msiba mbona hamsemi? Waongo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Nalipongeza Bunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wake wa Kikatiba wa kutunga sheria, lakini pia kwa kuishauri na kuisimamia Serikali inapotekeleza majukumu yake ya Kikatiba. Kwa ujumla nawashukuru Wabunge wote kwa ushirikiano mnaopatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali nchini. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Msiba.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefiwa.

*(Hapa vipaza sauti vilizima)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Naona kipaza sauti kimezima.

**MBUNGE FULANI:** Tuna Msiba.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Tuna msiba hatutaki, ahaa!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Uongozi ambacho ndicho chombo cha mamlaka ya juu, sasa hivi iko kwenye session na itatuletea majibu kwa muda mfupi, tuvumilie na Kiti kitaongozwa na Kamati ya Uongozi na baada ya hapo tutatoa maagizo mengine.

**MBUNGE FULANI:** Watu hawasikilizi.

**MBUNGE FULANI:** Msiba!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa AG hebu kaa kwanza.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Serikali sikivu na Kiti sikivu, nasitisha Bunge kwa muda wa dakika 15. *(Makofi)*

*(Saa 5.14 Asubuhi Bunge lilisitishwa kwa dakika 15)*

(Saa 5.51 Asubuhi Bunge lilirudia)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. CHARLES MLOKA- KATIBU MEZANI:**

### **HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mkataba wa Ubia wa Uchumi baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya (*Economic Partnership Agreement between the East Africa Community partner States and European Union (EAC - EU, EPA)*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwasomea Kanuni ya tano (5) ya Kanuni zetu, Kamati ya Uongozi imekaa na maamuzi ya Kamati ya Uongozi yataelekezwa kwenye Kanuni yetu ya tano (5), ambayo inasema hivi:

“Katika kutekeleza majukumu yake yaliyotajwa katika Ibara ya 84 ya Katiba, Spika ataongozwa na Kanuni hizi na pale ambako Kanuni hizi hazikutoa mwongozo, basi Spika atafanya kazi kwa kuzingatia Katiba, Sheria nyingine za nchi, Kanuni nyingine zilizopo, maamuzi ya awali ya Maspika wa Mabunge pamoja na mila na desturi za Mabunge mengine yenye utaratibu wa Kibunge unaofanana na utaratibu wa Bunge la Tanzania.”

Kutokana na hoja ya asubuhi ya msiba, Kamati ya Uongozi imefanya maamuzi na imeridhia kuwa Bunge hili kutokana na heshima ya Mheshimiwa Sitta tuliahirishe. Kwa hiyo, naomba sasa Waheshimiwa subirini kidogo mambo...

Mheshimiwa AG tunakwenda kwa Kanuni, naomba uje utoe hoja ili hati iliyowasilishwa mezani iweze kujadiliwa. (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, hati iliyowasilishwa mezani kwako asubuhi hii na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara ijadiliwe.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 5.57 Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,  
Tarehe 8 Novemba, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*